Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumatatu Novemba 20, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581500
nipasheTZ nipasheTZ
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com




SABABU 5 LIVERPOOL KUWA NA WASIWASI MSIMU HUU

UKURASA 12

UKURASA WA 2
**Chatanda** ahamasisha wanawake kumuunga mkono Samia 2025



UKURASA WA 7
**Neno** 'mhudumu' lasababisha kifo mmiliki wa baa



# Makaburi yaliyojaa yageuzwa dili mjini

• **Vigogo** watajwa, familia zachangia kaburi...

*Endelea ukurasa 4*



Baadhi ya wafanyakazi kwenye makaburi ya Sinza, Dar es Salaam, wakimwonyesha mteja eneo la kuzika ndugu yake licha ya makaburi hayo kutangazwa na serikali yamejaa. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3
### MWANDISHI WA NIPASHE SIMIYU AFARIKI DUNIA
MWAKILISHI wa Habari wa gazeti la Nipashe Mkoa wa Simiyu, Happy Severine...

UKURASA WA 8
### NSSF YAPONGEZWA MATUMIZI TEHAMA DARAJA LA NYERERE
MIFUMO ya TEHAMA iliyofungwa katika mradi wa Daraja la Nyerere, Kigamboni...



UKURASA WA 19
### NCHI TANO ZAPELEKA HOJA ICC DHIDI YA ISRAEL
NCHI tano miongoni mwa zilizotia saini kuhusu kuundwa kwa Mahakama ya...

## ZEC kuanza uandikishaji wapigakura wapya Pemba

UKURASA 3



## Washtuka ujenzi kituo cha polisi kugharimu mil. 802/-

UKURASA 2

MICHEZO GAMONDI AIANDALIA 'SAPRAIZI' BELOUIZDAD UK.24 KATUNI UK.6




Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na mgeni wake Rais wa Romania, Klaus Iohannis, Ikulu jijini Dar es Salaam jana katika hafla ya kumuaga baada ya kukamilisha ziara yake nchini. **PICHA: IKULU**

# Minong'ono yaibuka ujenzi kituo cha polisi kugharimu milioni 802/-

**Na Vitus Audax**

BAADHI ya wananchi wa ndani na nje ya Wilaya ya Butiama, mkoani Mara, wamehoji uhalali wa ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja B cha Wilaya ya Butiama mkoani Mara kugharimu zaidi ya Sh. milioni 800.

Katika hoja yao, baadhi ya wananchi hao wanaitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufanya uchunguzi kuhusu utekelezaji wa mradi huo.

Ni baada ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambaye ni Mbunge wa Butiama, Jumanne Sagini, kukagua mradi huo na kubainishwa kuwa ujenzi wake unatarajiwa kugharimu Sh. milioni 802.

Mmoja wa wananchi hao, Godlisten Mbaraka, alisema kuwa baada ya kusikia gharama zinazotumika kujenga kituo hicho na kulinganisha na mwonekano wake, anaona haulingani na thamani ya fedha.

"Labda kama kuna ujenzi mwingine uliofanyika kwa ndani kama maandaki, ujenzi wa nyumba za askari na mambo mengine, lakini kwa mwonekano wa nje huu tunaoona, mradi haundendani na thamani ya fedha," alidai.

Naibu Waziri Sagini akiwa katika ziara ya kikazi wilayani humo hivi karibuni, alitembelea na kukagua ujenzi wa kituo hicho na kuonesha kuridhishwa na utekelezaji wake.

Alimwagiza mkandarasi kukamilika kwa wakati mradi huo ulioko katika eneo la Mtuzu, Kata ya Butiama ifikapo Desemba mwaka huu kama ilivyoelekezwa.

Meneja wa mradi huo kutoka Kikosi cha Polisi Ujenzi, SP Masiva Mfinanga, akitoa taarifa ya utekelezaji wake, alisema mradi huo una thamani ya Sh. milioni 802. Ujenzi ulianza Mei 6 mwaka huu na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi ujao.

Taarifa hiyo iliibua mjadala katika mitandao ya kijamii, wachangiaji wakilinganisha picha ya kituo hicho iliyowekwa mtandaoni na kiasi cha fedha kinachotajwa huku wakishinikiza uchunguzi kufanyika.

Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mara, Antony Gang'olo, akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu kuhusu utekelezaji wa mradi huo, alisema kuwa kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba mwaka huu, kituo hicho hakikuwa kwenye miradi iliyofanyiwa ufuatiliaji, hivyo hakuwa na taarifa zake.

"Kwa sasa taarifa za kituo hicho sina, lakini tunaweza kuwa tulikifanyia ufuatiliaji katika kipindi cha nyuma, hivyo kesho (leo) nikiwa ofisini nitapitia taarifa za nyuma ili nione kama tulifuatilia, tulibaini nini na kushauri nini ili nikupe taarifa kamili. Kwa sasa siwezi kulielezea chochote," alisema Gang'olo.

Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda, katika taarifa yake kuhusu suala hilo jana, alibainisha kuwa mpaka jana serikali ilikuwa imetoa Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho. Kati yake, Sh. milioni 366 zilishatumika.

Alisema kituo kina ofisi za OCD, OCCID, DTO na OCS. Kina mahabusu sita zikiwamo za watoto chini ya miaka 18 (mbili); mahabusu ya wanaume na wanawake na watu wenye ulemavu. Zina uwezo wa kuchukua watu 50 hadi 60. Kituo kina jumla ya vyumba 31 na vyoo 15.

Mtanda alisema watakagua kupitia Mkaguzi wa Ndani takwimu na kiasi cha fedha kilichotumika kama kinalingana na thamani ya fedha na wataishauri serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi mradi huo unaweza kuisha chini ya thamani hiyo iliyotajwa.

"Mwisho, eneo linahitaji uzio na canteen, endapo fedha iliyopitishwa kwenye bajeti itatolewa, tuombe kibali cha kutekeleza sehemu ya pili ya mradi," alisema.

**TANGAZO! TANGAZO! TANGAZO !**

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA KUJITOLEA KATIKA TAAISI BINAFSI (WATO CO. LTD MOSHI) WANAHITAJIKA WAFANYAKAZI WAFANI ZIFUATAZO KATIKA MIKOA YOTE NDANI YA TANZANIA.

> **Uhasibu**
> **Afisa masoko**
> **Dereva**
> **Ulinzi Usafi**

1. Umri kuanzia miaka 18 hadi 45
2. Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea .
3. Muombaji aambatanishe malezo binafsi (cv) pamoja na nakala za vyeti zilizo thibitishwa na mwanasheria.
4. Muombaji aambatanishe na barua ya utambulisho ya serikali za mtaa husika

**MAELEZO YA JUMLA**

BARUA ZA MAOMBI YA KAZI PAMOJA NA WASIFU (CV) ZITATUMWA / ZITUMWE KWA EMAIL ADDRESS

**Jobsvoluntary@gmail.com**
**paulmassawe7@gmail.com**
**Mob : 0736 261 301,0710254032**

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 8/12/2023**

# Chatanda ahamasisha wanawake kumuunga mkono Samia 2025

**Na Christina Mwakangale**

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake Taifa (UWT), Mary Chatanda, amewahamasisha wanawake nchini kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan ili achaguliwe kiti cha urais mwaka 2025.

Amesema fursa za uongozi wa juu hasa kwa wanawake ni nadra kutokea, nafasi iliyopatikana kwa kundi hilo isiachwe kwa kumuunga mkono Samia arudi katika urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Chatanda ambaye ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam, kwenye hafla ya kumkabidhi tuzo Balozi Getrude Mongella, iliyotolewa na Tapo la Umajumui wa Wanawake wa Kiafrika (PAWO), kutambua mchango wake ujenzi wa harakati kumkomboa mwanamke.

Mgeni rasmi katika tuzo hiyo iliyohudhuriwa na baadhi ya viongozi wanawake kutoka taasisi mbalimbali, alikuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima.

"Amekwenda Beijing (Mongella) tumemtuma, amerudi amefanikiwa tumefika tumepata hii nafasi tusiiachie kumuenzi Mama Mongella ni kuhakikisha Rais Samia anarudi tena kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

"Tulienda Beijing kudai na sisi tunahitaji tuwe katika nafasi za uongozi wa juu. Mimi najua hata Suzan Lyimo (wa CHADEMA) tuko pamoja katika hili katika jambo, tusimamie pamoja, ili mradi ni la mwanamke ni ajenda ya mwanamke tumepata nafasi tusiiachie," alisema.

Chatanda alisema anatambua mchango wa Mongella na atajitahidi kufuata nyayo zake hasa za kuhakikisha wanawake wanapata mafanikio kisiasa, kiuchumi na kijamii.

"Tutaendelea kukuita kungwi, mwanaharakati wa kijinsia, mwanamke wa mfano," alisema Chatanda.

Pia alifikisha kilio chake kwa Dk. Gwajima, cha ongezeko la ukatili wa kijinsia hususan vitendo vya ubakaji kwa wanawake na matukio ya ulawiti.

"Kila tunapofanya mikutano tunakutana na taarifa za ubakaji, ulawiti. Tutoe elimu na kushirikiana kupiga vita, jambo hili hali ni mbaya, tunakutana na wanawake walionyanyaswa na kulawitiwa watoto wetu," alisema Chatanda.

Awali, Dk. Gwajima alisema wanawake wana deni la kushikilia sawa ajenda yao kwa kushikilia haki zao kwa kutengeneza wanawake kuwa viongozi wengi zaidi.

"Kama miaka 60 ilikuwa haitosi kukaa kwenye kilele cha Beijing, je, miaka mitano tu itoshe kukaa kwenye ulingo wa Beijing? Twende mbele na Samia, twende tena, twende. Tuzo yetu tutapewa kwa kumweka Rais mwanamke," alisema Dk. Gwajima.

Alikumbusha viongozi wanawake wameikuta historia ya Mongella, wataendelea kuisimulia na kushawishi wajao, ili ibaki kwenye kumbukumbu kwa ajili ya vizazi vijavyo.

"Tunatambua hata sisi wanawake viongozi kufikisha hapa kuna mchango wa Getrude Mongella. Uamini kwamba yanawezekana, wanapostaafu viongozi kama hawa tutambue sisi tunaweza kushika maono yao," alisema Dk. Gwajima.

"Juhudi zake zimeleta matunda. Tuzo hii ni chachu kwa wanawake wengine kuwania nafasi za uongozi, serikali ya Rais Samia inaendelea kujenga mazingira wezeshi ya kuwawezesha wanawake kiuchumi," alisisitiza.

Kuhusu matukio ya ukatili wa kijinsia, Dk. Gwajima alisema kunahitajika mjadala wa kitaifa, akisema wanaume wanahitaji kuhusika zaidi kwenye majadiliano hayo, kuleta mabadiliko kwenye jamii.

"Hali sio nzuri, tunahitaji mjadala, wanaume waungane na wanawake kupinga matukio hayo. Ila tunahitaji kubadili fikra katika jamii kwamba mtenda kosa hilo aionee aibu jamii. Wanaweza wakabadilika," alisema Dk. Gwajima.

Katibu Mtendaji wa PAWO, Dk. Susan Kolimba, alisema tuzo kama hiyo hutolewa kwa watu mbalimbali ambao huwa mstari wa mbele kusimamia haki na ajenda ya mwanamke, kama vile marais barani Afrika na mawaziri na viongozi wa mashirika na taasisi.

HABARI KITAIFA

# Biteko ataka TANESCO isilale hadi wananchi wapate umeme

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (pichani), amesema Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) halitalala usingizi mpaka wananchi wapate umeme.

Biteko alitoa kauli hiyo hivi karibuni wakati akizungumza na shirika hilo na kueleza kuwa, wamechukua mamlaka yote mikoani na kuyarundika makao makuu (TANESCO) huku kukiwa hakuna wanachofanya.

"Ninataka niwahakikishie TANESCO hamtalala. Hamtalala usingizi mpaka wananchi wamepata umeme.

Kama hamtafikiri, tutawasaidia kufikiri. Kama tutawasaidia kufikiri sisi, tutatumia kila aina ya nguvu kulinda uhalali wetu kwa wananchi kwa kuwapelekea umeme," alieleza.

Dk. Biteko alisema ni kweli yapo matatizo yaliyo nje ya uwezo wa shirika, lakini yapo ambayo yako ndani ya uwezo wao.

"TANESCO niliwaambia jana na ninarudia kuwaambia, kama kweli asilimia 65 ya umeme wa nchi hii ni wa gesi, na gesi haitoki mahali kwingine, inatoka Mtwara na Lindi.



"Kwenye kituo chetu cha gesi hapa, kuna mashine imeharibika miaka miwili, haijatengenezwa. Ukiwauliza TANESCO wanakuambia, 'taratibu za manunuzi'. Pili TANESCO mmechukua mamlaka yote mikoani mmejirundikia makao makuu, hakuna mnachofanya," alisema na kuongeza: "Kitengo cha Uniti ya manunuzi pale TANESCO mjiangalie sana, ninakuja huko, hatuwezi wananchi wanalia umeme sisi eti tumejificha kwenye neno linaloitwa taratibu za manunuzi, Mkurugenzi ninafurahi upo hapa, ninataka tufanye juu chini hili jambo la umeme hata kabla ya Bwawa la Mwalimu Nyerere kuingia maana sasa tunasubiri Mwalimu Nyerere kuingia." Dk. Biteko alisema anataka wamalizane na hao watu mapema huku akiahidi kuwa, wataiangalia upya menejimenti ya shirika hilo ili kutafuta ambao wanajua ukubwa wa tatizo.

"Watu ambao inawauma. Ni kweli wanafanya kazi nzuri sana, lakini wale wachache wanaowarudisha nyuma jiangalieni kabla sijaja mimi. Jipitieni, pitisheni macho muangaliane namana mnavyoishi, nilichokiona Mtwara inawezekana ni sampuli tu ya hali halisi ya nchi zima. Ninatamani TANESCO iwe ni kimbilio la watu.

Septemba 27, mwaka huu, baada ya Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Gissima Nyamo-Hanga, kuteuliwa katika nafasi hiyo, aliainisha mikakati mbalimbali, ili kukabiliana na kiwango cha upungufu cha megawati 400 kuwa watakipunguza kwa wastani wa megawati 100 kwa kila mwezi.

Nyamo-Hanga alisema matarajio ya shirika ni hadi mwishoni mwa mwezi Machi, mwaka 2024, tatizo liwe limekwisha kwa kuwa, watakuwa wamekamilisha matengenezo ambayo yanaendelea kwa mitambo na visima vya gesi asilia.

# Mwandishi wa Nipashe Simiyu afariki dunia

**Na Ndalike Songa,** SIMIYU



MWAKILISHI wa habari wa gazeti la Nipashe Mkoa wa Simiyu, Happy Severine (pichani) amefariki dunia wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) jijini Dar es Salaam.

Taarifa kuhusu kifo cha mwandishi huyo aliyeugua kwa muda mrefu ilithibitishwa jana na dada wa marehemu, Alice Luhoga aliyekuwa anaishi naye jijini Dar es Salaam wakati akiendelea na matibabu.

Luhoga aliiambia Nipashe kuwa Happy alifariki dunia usiku wa kuamkia jana wakati akiendelea na matibabu ya ugonjwa wa mapafu uliokuwa ukimsumbua kwa muda mrefu.

Alisema taratibu za mazishi zinaendelea wakati wakimsubiri mume wa marehemu aliyekuwa safarini jana akitokea mkoani Simiyu kuelekea Dar es Salaam, ili kupanga rasmi siku na eneo yatakakofanyika maziko.

Kufuatia msiba huo, vilabu vya waandishi wa habari kutoka mikoa ya Mwanza na Simiyu vimetoa salamu za pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa Happy na kueleza kusikitishwa na kifo cha mwandishi huyo.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Simiyu (SMPC), Frank Kasamwa, alieleza kupokea msiba wa Katibu Mtendaji wa Klabu hiyo, Happy, kwa majonzi na kuwataka waandishi, ndugu, jamaa na marafiki kuendelea kuwa wavumilivu katika kipindi chote cha majonzi.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Mwanza (MPC), Edwin Soko, alitoa salamu za pole kwa niaba ya waandishi wa habari mkoani humo na kusema mwanachama huyo na kiongozi katika Klabu ya Simiyu alikuwa na mchango mkubwa katika kuinua na kukuza tasnia ya habari.

Akizungumza na Nipashe, Katibu Msaidizi wa SMPC, Derrick Milliton alisema Happy alikuwa anatibiwa katika hospitali mbalimbali mkoani Simiyu kabla ya kupelekwa Muhimbili mwanzoni mwa mwezi Septemba mwaka jana.

# ZEC kuanza uandikishaji wapigakura wapya Pemba

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), inatarajia kuandikisha wapiga kura wapya 162,606 ikiwa ni maandalizi ya uchaguzi mkuu ujao wa 2025.

Mwenyekiti wa ZEC, Jaji George Joseph Kazi, ameomba ushirikiano kati ya wananchi, vyama vya siasa na wadau wote wa uchaguzi ili kufanikisha maandalizi hayo yanayotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Akizungumza katika mkutano uliowashirikisha wananchi na wadau wa uchaguzi kisiwani Pemba, Jaji Kazi alisema uandikishaji huo ni kwaajili ya wapigakura wapya pekee na kuwataka wadau watoe ushirikiano ili mwananchi apate haki yake ya kujiandikisha ya kuwa mpigakura.

Alisema takwimu wanazotarajia kuandikisha ni kwa mujibu wa taarifa walizozipata katika sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

Alisema huo ni uandikishaji wa awamu ya kwanza na baadaye itafanyika awamu ya pili.

Jaji Kazi alisema uandikishaji utaanza katika kisiwa cha Pemba Wilaya ya Micheweni kuanzia Desemba 2 na kumalizia Wilaya ya Mkoani Desemba 14 na baadaye utaendelea Unguja Desemba 23 katika Wilaya ya Kaskazini 'A' na kumalizika Januari 15, mwaka 2024.

Uandikishaji utafanyika kwa siku tatu katika kila kituo kilichopangwa na Tume na vituo vitafunguliwa kuanzia saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 10 jioni.

Akizungumza na wadau, Kaimu Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba na Mkuu wa Wilaya Wete, Dk. Hamad Omar Bakar, aliwataka wadau hao kushiriki.

Wakitoa maoni yao, baadhi ya washiriki wameomba Tume kuendesha uandikishaji huo kwa uaminifu .


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA

*Dar es Salaam, Novemba 20, 2023*

**TAARIFA KWA UMMA**

**UTAPELI MITANDAONI KUHUSU HUDUMA ZITOLEWAZO NA NIDA**

Kumekuwepo na wimbi la utapeli linalofanywa na watu wenye nia ovu ya kujipatia fedha kutoka kwa wananchi isivyo halali kwa kuweka matangazo katika mitandao ya Kijamii kuwa wanatoa ***Namba za Utambulisho wa Taifa (NIN), Vitambulisho vya Taifa na Nakala tepe mtandaoni (Online Soft Copy).*** Baadhi yao wametengeneza Akaunti bandia (fake) za Mitandao ya Kijamii ya Mamlaka na hujitangaza kuwa wanatoa huduma hizo kwa niaba ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na kuwataka wanaohitaji huduma hizo kulipa fedha kupitia namba za simu za mkononi.

Tunawatahadharisha wananchi kujiepusha na watu hao kwani NIDA ndiyo taasisi pekee yenye Mamlaka kisheria ya kutoa huduma hizo na haina wakala au mtu yeyote inayeshirikiana naye kuchapisha na kutoa Namba na Vitambulisho vya Taifa. Aidha, NIDA haina huduma ya Nakala tepe mtandaoni (Online Soft Copy).

Tunawakumbusha wananchi kuwa malipo kwa taasisi za Serikali ikiwemo NIDA hufanywa kupitia Namba ya Malipo ya Serikali (Control Number) na si kupitia namba za simu za mkononi hivyo, endapo mtu yeyote atakutaka kulipia huduma yeyote ya **NIDA kupitia namba ya simu ya mkononi, hayo si malipo halali ni UTAPELI.**

Tunatoa rai kwa wananchi kutumia njia na taratibu sahihi zilizowekwa na Mamlaka katika kupata huduma zetu za Usajili na Utambuzi ikiwa ni pamoja na kutumia ofisi zetu za Usajili badala ya kutumia njia za mkato.

**Imetolewa na:**

**Kitengo cha Mawasiliano**
**MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA**

**Barabara ya Kilimani, S.L.P 12324, Dar es Salaam, Simu: +255734220962,**
**Barua pepe: info@nida.go.tz, Tovuti: www.nida.go.tz**

RIPOTI MAALUM

# Makaburi yaliyojaa yageuka dili mjini

## -Vigogo watajwa, familia zachangia kaburi...

**Beatrice Shayo na Restuta James**

NI miaka mitano sasa tangu serikali itangaze kujaa kwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kuzika mkoani Dar es Salaam, lakini baadhi ya maeneo hayo yanaendelea kutumika kwa maziko.

Uchunguzi wa Nipashe umebaini kuwa gharama za maziko katika maeneo ya jiji ni kuanzia Sh. milioni 1.2 hadi Sh. milioni 1.8 kwa kaburi la kujengwa kwa zege na Sh. 300,000 hadi Sh. 600,000 kwa lisilojengwa kwa zege.

Waandishi wa habari hizi wamebaini kuwa madalali ndio hutumika kutangaza kuwapo nafasi za kutosha na kupanga bei.

Uchunguzi wetu umebaini kuwa makaburi ya Kinondoni, Sinza, Kisutu na Magomeni yameendelea kutumika kwa shughuli za maziko licha ya serikali kutangaza yamejaa mwaka 2018.

Mathalani, katika eneo la makaburi ya Kinondoni, waandishi wa habari hizi walifika na kuomba eneo la kaburi na kutakiwa kulipia Sh. milioni 1.8 kwa kaburi la kujengea au Sh. 600,000 kwa kaburi lisilojengwa.

"Unatakiwa ulipe hela (fedha) mapema ili sisi tuwaandalie kaburi maana ukichagua hili la Sh. milioni 1.8 linahitaji walau siku moja ili likauke. Kama mnazika Ijumaa, ni vizuri leo (Jumatano) ukatuachia 'advance' (kianzio) ili tufanye kazi kesho (siku iliyofuata)," alisema mmoja wa wachimbaji wa makaburi katika eneo hilo.

Alisema masharti ya kupata eneo la kuzikia yanajumuisha kuoneshwa eneo na mtu akiridhia anafanya malipo ili maandalizi yaanze kwa kuwa hakuna mwanafamilia anayeruhusiwa kushiriki uchimbaji wa kaburi.

"Hapa eneo la kuzika lipo. Kama uko tayari tukupitishe uchague eneo na ikiwezekana ulipie kabisa ili tuanze kazi. Sisi ndio tunaochimba na kujenga. Ninyi mtaleta mwili, mtakuta kaburi lenu lipo tayari," alitamka kwa kujiamini.

Msimamizi wa Makaburi ya Manispaa ya Kinondoni, Nassib Rashid, alisema mwili wa kwanza kuzikwa katika makaburi hayo, ulizikwa mwaka 1938 na tayari yametangazwa kujaa miaka saba iliyopita.

"Makaburi yote yaliyopo katikati ya mji yamejaa. Si Kisutu, Buguruni, Ilala hata hapa Kinondoni pamejaa, lakini kuna familia chache zina maeneo hapa Kinondoni na nyingine zinazika kwenye kaburi moja baada ya kutuandikia barua," alisema.

Rashid alizitaja baadhi ya familia zenye maeneo ya maziko ni za Wabaha'i na Marehemu Balozi Paul Rupia.

Alisema eneo la maziko lililobaki katika makaburi ya Kinondoni ni kwa familia kuchangia kaburi moja baada ya kuwasiliana na ofisi yake.

"Unaona barua kama hizi familia imeomba kuzika kwenye kaburi moja nyingi ni zile baba ametangulia wanaomba kumzika pamoja na mama, hili huwa linatokea na hatuwezi kuzuia," alisema.

Kwa mujibu wa Rashid, manispaa inaruhusu kufukua kaburi na kuzika mwili mwingine juu ya ule uliozikwa awali kwa makubaliano ya wanafamilia.

Hata hivyo, alisema kupata eneo la kuzika katika maeneo yote ni bure, lakini zipo gharama za ujenzi kwa wale wanaotaka kujengea kaburi ambazo ni kati ya Sh. 700,000 hadi Sh. milioni 1.6.

"Sisi hatuuzi eneo la kaburi japokuwa kuna vishoka ambao wanawalaghai wananchi na kuwatoza fedha kama huyo uliyekutana naye. Gharama zilizopo ni za kuchimba kaburi na ujenzi na hilo ni suala la makubaliano ya nje na ofisi yangu," alisema huku akimtaka mwandishi ampuuze kijana aliyemtajia gharama.

Rashid alishauri wananchi wanapofiwa na wapendwa wao, waende Tegeta kwa Kondo wilayani Kinondoni kwa kuwa serikali imetenga eneo kubwa kwa ajili ya makaburi.

Alifafanua kuwa wakati mwingine anapata simu kutoka kwa aliowaita 'wakubwa' kuomba eneo la maziko. Wanalazimika kuwapatia kwa kuwa "mwenye nyumba ndiye anayejua wapi pa kumweka mgeni hata pale nyumba inapoonekana imejaa".



MAKABURI YA SINZA

Waandishi walizungumza na aliyejitambulisha mwangalizi wa makaburi ya Sinza. Alidai wana maeneo ya kuzika. Hata ukitaka kujenga kibanda kwenye kaburi la mpendwa wako inawezekana.

Alisema gharama za eneo la maziko zinazoanzia katika uchimbaji wa kaburi, ni kati ya Sh. milioni 1.2 na Sh. milioni 1.3 kwa kaburi la kujengea na Sh. 300,000 kwa lisilojengewa kwa watu wazima. Gharama kwa watoto ni Sh. 60,000 hadi Sh. 100,000 kulingana na umri.

"Twende nikakuonyeshe eneo uchague. Mbona juzi tu tumezika maiti mbili, bado hapajaja, huwa wanaongea raia tu... nafasi zipo nyingi sana hata zije maiti 10 kwa siku moja zinapata nafasi zitazikwa," alisema.

Mwangalizi huyo alifafanua kuwa anayehitaji kupatiwa eneo, ni shari alipe walau nusu ya gharama hizo kabla uchimbaji kaburi haujaanza. Kiasi kingine kinalipwa siku ya maziko.

"Cha kufanya kwa sasa tupatie Sh. 10,000 kwa ajili ya 'booking' (kuweka nafasi) ya uwanja na kesho uje kulipia hizo fedha za kaburi... ukilipa 'advance' tunaanza kazi ya kununua matofali, saruji, mchanga, maji na kuanza kujenga kaburi, kuweka floor (sakafu) na plasta, kazi yenu ni kuja na kuzika tu, sisi tunawatayarishia kila kitu," alisisitiza.

"Hapa hapajajaa, kesho (siki iliyokuwa inafuata) yenyewe kuna watu wanakuja kuzika na kaburi lao linaanzia chini, wanataka kujengea. Sisi wote 10 hapa ni wachimbaji, tumewekwa chini ya serikali ya mtaa, twende tukakuoneshe maeneo uchague mnapotaka kuzika tuanze maandalizi."

Tofauti na makaburi mengine ya mjini, mwangalizi huyo ambaye hakutaka kutaja jina lake, alisema wanafamilia wanaweza kujenga kibanda cha kutunza kaburi la ndugu yao kwa kibali ambacho kinatolewa bila gharama katika ofisi ya serikali ya mtaa.

Waandishi wa habari hizi walipelekwa kuoneshwa maeneo matatu kwa ajili ya kuzika huku waelekezaji wakiwa na tepu za kuchukua vipimo vya kaburi. Kwa kaburi la mtu mzima ni mita tatu kwa saba.

### KWA KONDO

Msimamizi wa makaburi ya Tegeta Kondo, Hamisi Kisomi, alibainisha eneo hilo ni kubwa na lilianza kutumika miaka tisa iliyopita.

"Tulihamisha mabaki ya mifupa kutoka Ilala wakati wanapitisha barabara yakaletwa hapa na wenye ndugu walipatiwa taarifa na hayo makaburi ya chini unayoyaona ni ya waliofariki kwa ugonjwa wa UVIKO-19, huu uwanja ni mkubwa," alisema.

Alibainisha gharama za kaburi katika eneo hilo ni Sh. milioni 1.4 hadi Sh. milioni 1.6 kwa makubauri ya kujengewa na Sh. 300,000 kwa yasiyojengwa.

"Kuna hili kaburi chini limejengewa na ndani ya kaburi udongo haujaingia, shimo linajengwa la futi tisa na upana futi tatu na juu ni mfuniko wa zege, ndani wanaweka marumaru na pembeni pia. Gharama zake ni Sh. milioni 1.6," alifafanua.

Msimamizi huyo alibainisha kuwa kwa sasa watu wengi wanazika wapendwa wao bila kufukia kwa mchanga.

"Hawa wanaojengea makaburi ni vigumu kwa baadaye kulikosa kaburi kama ilivyo kwa makaburi ya huko mjini ambao hawajajengea makaburi yao," alisema.

Kuhusu kujenga kibanda juu ya kaburi, msimamizi huyo alisema amepatiwa maelekezo kwa sasa utaratibu huo hautakiwi na waliofanya hivyo awali, walikosea.

"Hao walioweka vibanda wamejenga kwa makosa. Hapa nina siku tano nimepewa barua ya kuzuia vibanda kujengwa kwenye makaburi.

"Kujengea kaburi ni sawa, lakini huu mfumo mpya umekuja juzi wa kuzuia vibanda visiendelee, nimeletewa zuio la vibanda visiendelee," alisema na kubainisha maandalizi ya makaburi yanafanywa ofisini kwake, mwisho wa kuzika ni saa 12:00 jioni.

"Kama amefariki (dunia) nyumbani, utatakiwa kutupatia barua ya Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, kama amefariki (dunia) akiwa hospitalini tutatumia kibali cha hospitali. Ninyi si mna kibali cha hospitali?" alihoji kwa waandishi wa Nipashe waliozuru huko kwa ajili ya uchunguzi.

Katika maeneo yote ya makaburi ambako waandishi wa Nipashe walitembelea, wachimbaji hawakuwa tayari kutaja majina wala namba zao za simu. Badala yake walitaja namba za watu walio jirani na eneo la makaburi.

### KUTOKA KWA MEYA

Aliyekuwa Meya wa Manispaa ya Ubungo, Bonifance Jacob, alisema halmashauri ilishatoa uamuzi wa kusitisha kuzika katika makaburi ya mjini tangu mwaka 2018 kwa hoja kwamba yote yamejaa.

Alisema kuendelea kuzika katika maeneo yaliyojaa kunachangiwa na mambo mengi, ikiwamo madalali na baadhi ya viongozi wa serikali kulazimisha maziko kwenye maeneo hayo.

Alisema makaburi ya Kinondoni, Sinza, Mwananyamala, Kimara Baruti, Mburahati, Magomeni, Ubungo Maziwa na mengine yote ya mjini yamejaa. Kinachofanyika huko kwa sasa kinakinzana na maelekezo ya halmashauri.

Alishauri serikali iweke mkakati wa kuzuia watu kuzikwa mjini ili kuzuia uwezekano wa kuharibu makaburi ya awali.

### WATENDAJI SERIKALINI

Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi Manispaa ya Kinondoni, Ramla Mwasha, alisema makaburi ya mjini yote yamejaa. Wananchi wanapaswa kwenda kuzika wapendwa wao katika maeneo mapya ya Kondo, Mbweni, Bunju na Mabwepande.

Alisema eneo la Kwa Kondo lina ukubwa wa hekta 11.4, Mbweni hekta 11, Moga Bunju hekta 1.34 na Mabwepande hekta 16.71. Kunahitajika kujengewa uzio, taa na ulinzi ili kuzuia watu kuyavamia.

Alisema makazi yote yaliyopimwa yana maeneo ya makaburi pamoja viwanja vya shule, zahanati na nyumba za ibada, lakini watu wanapenda kuzika makaburi ya mjini kuliko na huduma muhimu za kijamii.

Ofisa Afya wa Manispaa hiyo, John Kijumbe, aliwaambia waandishi wa Nipashe kuwa maeneo yote ya makaburi yako salama. Hakuna makaburi yanayofukuliwa.

Katika uchunguzi huo, waandishi wa habari hizi pia wamebaini kuwa watu waliozikwa katika makaburi ya Kinondoni ni pamoja na waliofariki dunia katika Vita vya Pili vya Dunia (WWII), wakiwamo raia wa Poland, waliozikwa kati ya mwaka 1942 na 1952.

## HABARI KITAIFA

# Kesi ya anayedaiwa kumshambulia jirani kwa nyundo yapigwa kalenda

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kinondoni inatarajiwa kuendelea kusikiliza kesi ya tuhuma za shambulio la mwili Desemba 7 mwaka huu inayomkabili mfanyakazi wa benki, Ibrahim Masahi, anayetuhumiwa kumshambulia kwa nyundo jirani yake Deogratus Minja.

Inadaiwa kuwa Masahi alimshambulia kwa nyundo jirani yake huyo baada ya Minja kwenda kumshtaki Serikali za Mitaa kwamba anatiririsha maji mchafu katika eneo lake.

Tarehe hiyo ilipangwa mwishoni mwa wiki na Hakimu Mkazi wa mahakama hiyo, Amos Rweikiza, baada ya upande wa mashtaka kutokuwa na shahidi wa kuendelea kutoa ushahidi katika kesi hiyo.

Wakili wa Serikali, Salma Jafari alidai kuwa shahidi ambaye alipangiwa kutoa ushahidi wake ni askari.

Alishindwa kufika mahakamani kutokana na kupangwa kusimamia Mtihani wa Taifa wa kidato cha Nne unaoendelea nchi nzima.

"Kwenye orodha hapa shahidi aliyetakiwa kuwapo leo kwa ajili ya kuendelea kutoa ushahidi ni askari polisi mpelelezi, hajafika kwa sababu yuko katika usimamizo wa mitihani ya kidato cha nne," alidai Jafari.

Baada ya wakili kudai hayo, Hakimu Rweikiza aliwaeleza upande wa mashtaka kwamba kesi hiyo inatakiwa kuendelea kusikilizwa kwa sababu inatakiwa kuisha kufikia Machi mwakani.

"Mshtakiwa, dhamana yako inaendelea hadi Desemba 7, 2023, upande wa mashtaka walete shahidi, kesi iendelee kusikilizwa," alisema Hakimu Rweikiza.

Masahi anatuhumiwa kuwa Januari 11 mwaka huu, akiwa eneo la Mbezi Msakuzi, ndani ya Wilaya ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam, alimpiga Deogratus Minja kwa nyundo na kumsababishia kupata madhara makubwa ya mwili mwake.

Katika ushahidi wake, Minja alidai kuwa tarehe hiyo, saa mbili na nusu usiku, alikuwa anapita nje ya geti la jirani yake Masahi, alimkuta kijana wa jirani huyo. Baada ya kumwona alizungumza kwa kilugha kwa sauti kubwa. Yeye hakuelewa.

"Ghafla kijana alikuja mbele yangu akanizuia nisipite, mara geti likafunguliwa akatoka Masahi akanihoji kwamba mimi ni kama nani na kwenda kumshtaki Serikali za Mitaa? Sikumjibu chochote, kijana wake akanipiga ngumi.

"Nilimgeukia jirani yangu ili amwonye kijana wake, lakini na yeye aliinua shati lake akatoa nyundo akanipiga nayo kichwani. Baada ya kupata maumivu makali nilianza kukimbia huku nikipiga kelele za kuomba msaada," alidai Minja.

Alidai kuwa baadaye alianguka chini ndipo Masahi akawa anamshambulia na nyundo mgongoni, maumivu yalipomzidi aligeuka, akampiga na nyundo kwenye mkono wa kulia na kwenye bega.

Alidai kuwa jirani yao alifungua geti na kumsaidia. Kwa kuwa alikuwa anavuja damu nyingi, walimpeleka Hospitali ya Bochi kwa ajili ya matibabu.

## NIDA yahadharisha utapeli mtandaoni

**Na Zanura Mollel**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imewatahadharisha wananchi kujiepusha na matapeli wanaotumia njia ya mtandao kwa kudai kufanya kazi za usajili na utoaji wa namba za NIDA kwa kuwatoza fedha kupitia mitandao ya simu ya mikononi.

Aidha, NIDA imesema jambo hilo ni kinyume na taratibu, na mamlaka haihusiki wananchi kutakiwa kuchukua tahadhari.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano cha NIDA, kuna wimbi la utapeli linalofanywa na watu wenye nia ovu kwa kutumia jina la mamlaka kwa madai ya utoaji wa Namba za Utambulisho wa Taifa (NIN), Vitambulisho vya Taifa na nakala tepe mtandaoni (online soft copy).

"Kumekuwapo kwa baadhi ya watu wanaotengeneza akaunti bandia (fake) za mitandao ya kijamii ya mamlaka na kujitangaza kutoa huduma hiyo kwa niaba ya mamlaka ya vitambulisho vya taifa (NIDA) huku wakiwataka wanaohitaji huduma hiyo kulipia fedha kupitia namba ya simu ya mkononi," ilisema taarifa hiyo.

Mamlaka hiyo imefafanua kuwa huduma zote za malipo ya serikali hufanyika kwa kupitia namba sahihi ya malipo ya serikali (control number), yanayofanyika kwa njia ya simu ya mkononi kwa madai ya kulipia huduma za mamlaka hiyo siyo sahihi, ni utapeli.

Aidha, NIDA imetoa rai kwa wananchi kutumia taratibu zilizowekwa na mamlaka hiyo kupata huduma za usajili na utambuzi, ikiwa ni pamoja na kutumia ofisi za mamlaka zilizopo maeneo mbalimbali nchini, na kusisitizwa kuepuka kutumia njia za mkato ambazo zimeonekana kutokuwa sahihi na kufanya upotoshaji kwa jamii ikiwamo matumizi ya mitandao ya kijamii kwa nia ovu.


AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
benki kwa maendeleo yako

TAARIFA KWA UMMA

Kuunganisha Matawi ya Kinondoni na Kijitonyama

Akiba Commercial Bank Plc. inapenda kuwajulisha wateja wake na umma kwa ujumla kuwa Benki itaunganisha matawi ya Kinondoni na Kijitonyama kuanzia tarehe 20/12/2023. Uamuzi huu wa kimkakati unalenga kuongeza ufanisi kwenye mtandao wetu wa matawi na kuboresha huduma kwa wateja wetu kupitia njia za kidigitali. Hivyo, akaunti zote zinazomilikiwa na wateja katika tawi la Kinondoni zitahamishiwa tawi la Kijitonyama lililopo jengo la Letsya Towers, barabara ya Bagamoyo.

Benki inawahakikishia uhamishaji usiokuwa na usumbufu wowote kwa wateja na wadau wa tawi la Kinondoni huku tukiendelea kutoa huduma bora kwa wateja.

Tunawashukuru wateja wetu wote kwa kutuchagua kuwa Benki yenu na kuendelea kutuamini. Tunajali sana uhusiano wetu na wateja na tunaahidi kuendelea kutoa huduma bora wakati wote.

Kwa maelezo zaidi, tembelea tovuti yetu **www.acbbank.co.tz**, kurasa zetu za mitandao ya kijamii au wasiliana na Meneja wa Tawi, Afisa Uhusiano au Kituo cha Huduma kwa Wateja kupitia nambari, **0746 811 510.**

**Utawala**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Stars pambaneni, tunataka kuwaona Kombe la Dunia

**KESHO** Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, itashuka tena dimbani kucheza mechi ya pili ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia 2026, zitakazofanyika katika miji 16 kwa ushirikiano wa nchi tatu, Marekani, Canada na Mexico.

Stars kesho itashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa kuikaribisha Morocco, baada ya Jumamosi kupata matokeo ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Niger kwenye mchezo wa kwanza wa Kundi E uliopigwa nchini Morocco.

Niger ilicheza mechi yake hiyo ya nyumbani nchini Morocco kutokana na uwanja wao kutokidhi vigezo vya Shirikisho la Soka Duniani, Fifa.

Licha ya kwamba kesho Stars itakuwa nyumbani, mchezo huo dhidi ya Morocco hautakuwa mwepesi kwao hata kidogo hasa kutokana na ubora walio nao wapinzani wao ukilinganisha na uliopita dhidi ya Niger.

Ikumkubwe katika kila kundi, timu itakayomaliza kinara, itafuzu moja kwa moja kushiriki fainali hizo ambazo kwa mara ya kwanza katika historia ya michuano hiyo tangu ianzishwe mwaka 1930, itaandaliwa kwa ushirikiano wa mataifa matatu.

Hivyo, haitakuwa mechi rahisi kwa Stars dhidi ya Morocco ambayo inapewa nafasi kubwa ya kuwa kinara wa Kundi E, linalozijumuisha pia Zambia, Congo na Niger.

Hata hivyo, huu ni wakati sasa kwa Stars kuonesha inaweza kukabiliana na kigogo yeyote hususan inapokuwa nyumbani kwa kupafanya kila timu inayotia mguu Uwanja wa Benjamin Mkapa haiondoki na pointi hata moja.

Hilo likiwezekana itaifanya kuvuna jumla ya pointi 12 nyumbani hivyo kuhamishia nguvu michezo ya ugenini ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kufuzu fainali hizo.

Licha ya kutambua ubora wa Wamorocco hao, sisi tunaamini kwenye soka lolote linaweza kutokea na kushangaza, hivyo Taifa Stars inachotakiwa ni kumheshimu mpinzani wake, lakini haina budi kupambana kufa kupona kwa dakika zote 90 bila kutazama ukubwa wao.

Jambo lingine faida kwa Stars kesho itakuwa nyumbani mbele ya mashabiki wake ambao tunaamini watalibeba vema jukumu la mchezaji wa 12 uwanjani, kwa kuishangikia mwanzo mwisho ili kuiongezea morali wa kufanya vizuri.

Katika hilo sisi tukiwa wadau namba moja wa michezo nchini, hatuna budi kuwakumbusha Watanzania wote kununua tiketi kwa wingi ili kwenda kuipa sapoti Taifa Stars kwa kushangilia mwanzo mwisho kuiwezesha kupata matokeo nyumbani.

Tunaamini Kocha wa Stars, Adel Amrouche pamoja na wasaidizi wake wamekiandaa vema kikosi chao kulingana na ukubwa wa mchezo huo, hivyo jukumu lililobaki ni kwenda kutekeleza yote waliyoelekezwa na kuonyesha juhudi binafsi katika kulipambania taifa.

Tunataka kuona kila mchezaji akipambana kufa kupona ili kuiwezesha Tanzania kufuzu kushiriki fainali za Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza katika historia ya michuano hiyo iliyoanzishwa mwaka 1930.

Nipashe tunaamini Stars inaweza kama kila mchezaji atakayeaminiwa na kupewa nafasi na kocha, atatambua amepewa jukumu kubwa la kuipambania jezi ya taifa na Watanzania zaidi ya milioni 60 waliopo nyuma yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Simba kucheza Ligi ya Mabingwa bila Kocha Mkuu ni aibu kubwa

**VIONGOZI** wa Simba wameendelea kufanya makosa juu ya makosa. La kwanza ni kumtimua aliyekuwa Kocha Mkuu, Robertinho Oliveira, kisa kufungwa mabao 5-1 dhidi ya Yanga.

Viongozi walimtimua au kumtoa kama 'kafara' kwa sababu wanachama na mashabiki wake walicharuka baada ya mechi ile. Wakajisahau kuwa na wao walipaswa wawajibiwe kwa kukosa kuwajibika kuelekea kwenye mechi ile ya watani wa jadi.

Kabla na baada ya mechi ile, kumekuwa na stori nyingi, zingine zikithibitishwa na wao wenyewe viongozi kuwa kufungwa kwao hakukuwa na mazingira ya kawaida na ikasababisha waseme watachunguza tuhuma juu ya baadhi ya wachezaji wake kufanya hujuma.

Rais wa zamani wa klabu hiyo, Ismail Aden Rage, naye alibainisha kuwa alikuwa na taarifa kwamba baadhi ya wachezaji hawakulala kambini siku ya kuamkia mechi hiyo.

Ukiachilia mbali hilo, zipo pia taarifa kuwa baadhi ya wachezaji wa timu hiyo hawataki kulala kambini, wamekuwa wakiondoka na kwenda kuishi majumbani.

Hapa sasa sijajua kama viongozi wanatambua hili, au la. Tangu Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa ianze kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wanachama na mashabiki kuwa wachezaji wa timu hiyo hawajitumi. Wanacheza kama wanaisaidia timu na si kama wanalipwa na kubeba mioyo ya mashabiki wanaosafiri na timu mikoa yote inayokwenda kucheza, hata nje ya nchi.

Sijawahi kusikia viongozi wamekaa na wachezaji na kuwaambia kinaga ubaga kuwa wabadilike na mtu ambaye anaona hawezi kupambana aondoke au avunje mkataba.

Badala yake baada ya hali kuwa mbaya, wanachama na mashabiki wamecharuka ndiyo Mwenyekiti Bodi ya Wakurugenzi, Salum Abdallah 'Try Again', anakuja kwenye vyombo vya habari na kusema mchezaji asiyejituma watamwondoa kipindi cha dirisha dogo la usajili.

Nadhani maneno haya yalipaswa akawaambie wachezaji kambini na baada ya hapo ndiyo aje aseme kuwa tayari ameshawaambia wachezaji wapambane.

Lakini kiongozi huyo ajue kuwa kipindi cha dirisha dogo hakina wachezaji wengi wazuri, hivyo hata kama kuwaondoa na kusajili watakuwa wachache sana, huku kwa jinsi hali ilivyo Simba inatakiwa isafishwe kwani kuna wachezaji ambao wanawafukuzisha makocha na kufanya kila mwalimu anayekuja Simba anaonekana mbovu, lakini watakapoondoka wanang'ara na kutamaniwa tena.

Kitu kingine kinachaoonesha baadhi ya wanachama na mashabiki kudai viongozi kutofuatilia kambi, inashangaza kuona mechi kubwa ya watani wa jadi hakuna udhibiti wowote kiasi cha haya yote yanatokea.

Sidhani kama kwenye kambi ya Yanga wiki moja kabla ya mechi eti mchezaji atoroke, kambi na wachezaji hawadhibitiwi. Hii ni tatizo, kwani mechi za watani wa jadi tangu enzi na enzi, timu yoyote ambayo haitakuwa na udhibiti wa kambi na wachezaji wake, basi itapoteza mechi hata kama ni bora kiasi gani.

Robertinho ni kama ametolewa kafara tu kuficha madhaifu ya viongozi. Robertihno ameondoka zake, mpaka sasa Simba inakwenda kwenye mechi dhidi ya Asec Mimosas bila Kocha Mkuu. Hilo ni kosa lingine. Kama ilikuwa ni ngumu kiasi hicho kwa nini ilimtimua kocha?

Fikiria hata kama kocha mpya akitangazwa leo Jumatatu, anaweza kuanza kuifundisha na mpaka Jumamosi akakaa benchi? Haiwezekani. Kuna mambo mengi atatakiwa kufanya kabla ya kuanza kukaa kwenye benchi la ufundi, ikiwamo kupata muda wa kufundisha, vibali vya kazi na ukazi.

Nadhani katika timu zote zinazoshiriki Ligi ya Mabingwa, Simba pekee ndiyo inayokwenda kuanza michuano hiyo bila kocha mkuu. Hii ni aibu kubwa kwa timu ambayo imecheza robo fainali nne za ligi hiyo.

Pamoja na kwamba Meneja Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally, anazunguka huku na kule kuhakikisha mashabiki wanajaa uwanjani, lakini baadhi wamekuwa na wasiwasi kutokana na hili la kutokuwa na kocha.

## ACT yataka tume utatuzi migogoro ardhi

**Na Julieth Mkireri,** KASULU

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali kuunda tume itakayoainisha migogoro ya ardhi katika maeneo yote nchini, hususani mipaka ya vijiji na hifadhi, ili itafutiwe ufumbuzi.

Tume hiyo itakuwa na wajibu wa kuwasikiliza wananchi wenye migogoro katika maeneo ya hifadhi ili baadaye ijulikane kiini cha tatizo na namna ya kulitafutia ufumbuzi na shughuli za wananchi zinazowaingizia kipato ziendelee.

Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe alitoa rai hiyo juzi alipohutubia mkutano wa hadhara katika Uwanja wa Kiganamo, mjini Kasulu, mkoani Kigoma.

Zitto ambaye yuko ziarani kutembelea majimbo ya uchaguzi ya Mkoa wa Kigoma, alisema tume hiyo inapaswa kuundwa na Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kuunda chombo hicho kama ilivyofanyika mwaka 1991.

"Lazima Rais aunde tume kama alivyofanya Rais mstaafu Ali Hassan Mwinyi mwaka 1991 ili kusikiliza kero na kupata maoni ya wananchi kuhusu masuala ya ardhi, hasa mipaka ya vijiji na maeneo ya uhifadhi," alisema.

Zitto alisema kuwa pamoja na mambo mengine, tume hiyo itasaidia kujua mahitaji halisi ya ardhi kwa ajili ya shughuli za kibinadamu, uhifadhi na mambo mengine ikiwamo uwekezaji na shughuli zingine za kiuchumi.

"Wananchi wasikilizwe na watu wa hifadhi pia wasikilizwe. Pale ambapo itakuwa lazima maeneo ya hifadhi kupunguzwa kukidhi mahitaji ya binadamu ni heri tufanye hivyo kwa sababu wajibu wa kwanza wa serikali ni maendeleo na maslahi ya watu (Ibara ya 8 ya Katiba ya nchi)," alisema.

Zitto alisema tatizo la mipaka kati ya vijiji na hifadhi linatakiwa kupatiwa ufumbuzi na serikali inatakiwa kushughulikia suala hilo haraka kwa kuunda tume itakayokuja na majibu.

Kiongozi huyo alisema kuundwa tume ya kushughulikia migogoro ya hifadhi na vijiji kutasaidia kupitia Sheria ya Ardhi ya Vijiji na kufanyia marekebisho ili sheria mpya itakapoundwa iendane na hali ya sasa.

Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Mkoa wa Kigoma, Sendwe Ibrahimu, alisema ipo migogoro kati ya wakulima na hifadhi. Wananchi wamekuwa wanazuiwa kufanya shughuli za kilimo katika maeneo hayo.

Ibrahim alibainisha kuwa katika Wilaya ya Uvinza, Kata ya Bulungu, hususan Kijiji cha Kalilani kinachopakana na Hifadhi ya Mahale, wananchi wametakiwa kuhama katika eneo hilo.

Alisema ni hali ambayo pia iko katika Kijiji cha Lukoma Kitongoji cha Mjimwema ambako wananchi wametakiwa kuhama kupisha mapito ya wanyama katika Hifadhi ya Mahale. Alilitaja ni jambo linaloendelea kuleta mgogoro kati ya pande hizo mbili.

Vilevile, alisema wananchi wa Kijiji cha Ilagala wana mgogoro na Jeshi la Magereza. Awali jeshi liliomba ekari 600 na sasa limeongeza hadi kufikia ekari 10,000 na hivyo wananchi kukosa eneo la kilimo.

Katika Mstitu wa Mkuti na Makere Kusini, kiongozi huyo wa ACT Wazalendo alisema kuna mgogoro unaoendelea kati ya wananchi na mamlaka za hifadhi.

Wakazi wa vijiji vya Lusesa, Kwaga, Rungwe mpya na Asante Nyerere wanazuiwa kuendelea na shughuli za kilimo wakidaiwa kuwa wanaingia eneo la hifadhi.

Mmoja wa Mawaziri Vivuli wa chama hicho, Julius Masabo, alisema ni vyema serikali ikayapitia upya maeneo hayo ili kutafuta ufumbuzi wa migogoro iliyopo kwa sasa.

Pia alisema kuna haja kuongeza maeneo kwa ajili ya kilimo kutokana na ongezeko la wananchi tofauti na miaka 30 iliyopita.

Sambamba na kutaka kuundwa kwa tume hiyo, chama hicho pia kimewataka viongozi wa vijiji wa chama hicho kuunda kamati kwenye maeneo yao zitakazosimamia utatuzi wa migogoro ili viongozi watakaochaguliwa katika uchaguzi ujao, wafanye kazi kwa ufanisi kwa kusimamia maslahi ya watu.

Mnamo mwaka 2019, Rais John Magufuli (hayati) aliunda Kamati ya Mawaziri Wanane akiipa jukumu mahususi la utatuzi wa migogoro ya ardhi.



Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani, Halima Okash (kushoto) na Mwenyekiti wa Taasisi ya Hassan Maajar Trust, Balozi Mwanaidi Sinare Maajar, wakikata utepe kuzindua jengo la darasa la kompyuta lililojengwa kwa msaada wa taasisi hiyo kwenye Shule ya Msingi Majengo Bagamoyo, mwishoni mwa wiki. Wa tatu kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa Hassan Maajar Trust, Sharif Maajar na walimu wa shule hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

KISA NENO 'MHUDUMU'

# Mmiliki wa baa adaiwa kuuawa na mteja wake

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MMILIKI wa baa ya Tale mjini Njombe, Jackson Mgeni (35), mkazi wa Mji Mwema mjini hapa, amefariki dunia kutokana na kuchomwa kisu tumboni na anayedaiwa mteja wake, Emmanuel Shiwa (32).

Shiwa, mfanyabiashara wa madini na mkazi wa eneo la Uwanja wa Ndege mjini Njombe, anadaiwa kutenda ukatili huo baada ya kutokea ugomvi kati yao alipomwita Mgeni, akitumia neno 'mhudumu'.

Ni tukio hilo lilitokea jana saa nane usiku katika baa hiyo ya mjini Njombe.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Alisema mtuhumiwa ni mteja mzoefu katika baa hiyo.

"Katika hali ya kupata huduma, mtuhumiwa alimwita Mgeni kwa jina la mhudumu. Sasa kile kitendo cha kuitwa mhudumu, ninafikiri kilimuudhi.

"Akaanza kugombana na yule mteja na yule mteja ninafikiri aliona hatoweza kupigana naye kawaida. Hivyo alitoka nje," alisema Kamanda Banga.

Aliendelea kusimulia, akisema: "Mtuhumiwa huyo baada ya kutoka nje alipanda gari lake, akaenda nyumbani kwake.

"Mashuhuda wanasema ni maeneo ya Uwanja wa Ndege, lakini baada ya muda alirudi na kisu na kumvizia yule jamaa na kumchoma nacho tumboni."

Kamanda Banga alisema kuwa baada ya kufanya tukio hilo, wananchi ambao ni wateja wa baa hiyo walikuwapo eneo la tukio, walimdhibiti mtuhumiwa na kutoa taarifa kituo cha polisi.

"Polisi walifika na kumkamata, majeruhi alikimbizwa Hospitali ya Halmashauri ya Mji Njombe (Kibena), lakini kabla ya kuanza kupatiwa matibabu alifariki (dunia)," alisema Kamanda Banga.

Njombe ni miongoni mwa mikoa yenye matukio mengi ya mauaji nchini.

Hata hivyo, matukio mengi yanahusishwa na imani za kishirikiana na wivu wa mapenzi.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



HABARI KITAIFA

# UTT AMIS yajigamba mifuko kukua kwa kasi

**Na Frank Monyo**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Uwekezaji ya UTT AMIS, Simion Migangala, amesema kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja ukubwa wa mifuko ya taasisi hiyo imekuwa kutoka Sh. bilioni 996.5 hadi kufikia Sh. trilioni 1.535 baada ya mifuko ya fedha kufunguka.

Migangala aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa Mkutano Mkuu wa mwaka wa Mifuko ya Uwekezaji ya taasisi hiyo, ambayo ni Mfuko wa Umoja, Mfuko wa Watoto, Hatifungani, Jikimu, Wekeza Maisha na Mfuko wa Jikimu.

Alisema kuwa ongezeko hilo la kiasi cha Sh. bilioni 538.9 ni sawa na asilimia 54.0 ikilinganishwa na ongezeko la Sh. bilioni 383.7 ongezeko hilo la ukubwa wa mifuko pamoja na kufunguka mifuko ya fedha pia imani ya wawekezaji, elimu itolewayo ya akiba na uwekezaji pamoja na faida shindani kwenye mifuko.

"Kwa kipindi cha mwaka mmoja, ukubwa wa mifuko umeongezeka kutoka Sh. bilioni 996.5, Juni 30, 2022 hadi kufikia Sh. trilioni 1.535, Juni 30, 2023. Ongezeko hili la kiasi cha Sh. bilioni 538.9 ni sawa na asilimia 54.0 ikilinganishwa na ongezeko la Sh. bilioni 383.7 ongezeko hili la ukubwa wa mifuko linatokana na imani ya wawekezaji kwetu, elimu itolewayo juu ya akiba na uwekezaji pamoja na faida shindani kwenye mifuko," alisema.

Migangala aliutaja Mfuko wa Umoja umekuwa kwa asilimia 11.2, Mfuko wa Wekeza Maisha asilimia 12.5, Mfuko wa Watoto asilimia 12.4, Mfuko wa Jikimu asilimia 14.0 ikilinganishwa na asilimia 7.6 ya kigezo linganifu. "Kwa mifuko iliosalia yenye uwekezaji kwenye maeneo yenye mapato vya kudumu faida kwa mfuko wa Ukwasi ni asilimia 12.5 na Mfuko wa Hatifungani ni asilimia 12.3 ikilinganishwa na asilimia 9.7 ya kigezo linganifu," alisema.

Kadhalika, kuhusu maendeleo ya Soko la Hisa, utendaji kwa kampuni za ndani ya nchi unapimwa kwa kuangalia mabadiliko ya Fahirisi (Tanzania Share Index) na katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2023, Fahirisi imeonyesha kuwa na ongezeko la asilimia 4.1 kutoka 3,928.5, Juni 30, 2022 hadi 4,091.8, Juni 30, 2023.

Mwenyekiti wa Bodi ya UTT AMIS, Casmir Kyuki, alisema katika Mpango Mkakati wa miaka mitano utakaoishia Juni, 2024, taasisi hiyo imeazimia kujikita kwenye matumizi ya teknolojia ya kutoa huduma kwa wawekezaji.

"Miaka minne iliyopita kampuni ya UTT AMIS ilizindua huduma ya uwekezaji kwa kutumia simu za kiganjani yaani UTT SimInvest (*150*82#), programu tumizi (UTT AMIS APP) na inaendelea kuunganisha mifumo ya benki na mifumo ya UTT AMIS. Lengo la uunganishwaji huu ni kuongeza ufanisi kwa kupunguza mlolongo wa hatua za uchakataji wa miamala inayofanywa kwa njia za benki," alisema.

Vile vile, hadi Juni 30, 2023, Meneja wa mifuko (UTT AMIS) ameunganisha mifumo yake na benki zifuatazo: CRDB, NMB, NBC na Stanbic huku CRDB akiendelea kuwa mwangalizi wa mifuko. Aidha UTT AMIS imeendelea na uunganishaji mifumo yake na benki nyingine.

"Ni matumaini yangu kuwa pindi zoezi hili la uunganishaji mifumo litakapokamilika, litaongeza idadi ya miamala inayofanywa kwa njia ya benki kwa asilimia kubwa zaidi. Pia huduma ya kuuza vipande kwa njia ya simu (SimInvest) imeanzishwa ambapo wawekezaji wanaweza kuuza vipande vyenye thamani hadi ya shilingi milioni mbili. Jitihada maalumu zimeanza kufanyika za kuwafikia Diaspora (Watanzania waishio nje ya nchi)," alisema.

Kyuki alisema kuwa kipindi cha miaka minne ya mwanzo ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Taasisi ya UTT AMIS utakaoishia Juni 30 2024, kumekuwa na mafanikio makubwa zaidi ya ilivyotarajiwa.

UTT AMIS inaendelea kuboresha namna ya uendeshaji wa mifuko ili iwe ya kisasa zaidi na kuhakikisha wawekezaji wanapata faida shindani kuendana na hali

## NSSF yapongezwa matumizi TEHAMA Daraja la Nyerere

**Na Mwandishi Wetu**

MIFUMO ya TEHAMA iliyofungwa katika mradi wa Daraja la Nyerere, Kigamboni jijini Dar es Salaam, imewagusa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC) na wameonesha kufurahishwa na hatua iliyochukuliwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kufunga mifumo hiyo.

Wakizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki wakati wa ziara yao katika daraja hilo, baadhi ya wajumbe hao akiwamo George Malima (Mpwapwa CCM), alisema wanaipongeza NSSF kwa kufunga mifumo ya TEHAMA katika mradi huo wenye tija kwa jamii na taifa.

"Tuwapongeze NSSF kwa usimamizi nzuri wa daraja hili, tumeona kumewekwa mifumo mbalimbali ya TEHAMA na magari hayachukui muda mrefu yakifika taratibu zinafanyika haraka za kulipia na kuondoka," alisema.

Pia, alisema mradi huo unaendana na kiwango cha fedha kilichotumika na umechangia maendeleo ya wananchi hususan wakazi wa Wilaya ya Kigamboni na watumiaji wengine kwa ujumla.

Naye Dk. Oscar Kikoyo (Mulemba Kusini- CCM) aliwaomba wananchi wa Kigamboni na watumiaji daraja hilo kutumia mifumo ya kidijitali iliyofungwa ikiwamo wa kulipa kwa bando ili kupunguza msongamano.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, alisema Mfuko kwa kutumia wataalamu wa ndani wa TEHAMA, umetengeneza mfumo wa makusanyo ya tozo ambao umeunganishwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya utambuzi wa magari wa kielektroniki wa malipo wa serikali (GePG).

"Mfumo huu unatoa fursa kwa wateja kuchagua aina ya huduma waipendayo ikiwamo malipo ya vifurushi (bundle), malipo ya kabla na mfumo wa fedha taslimu," amesema Mshomba.

Pia NSSF itaendelea kufanya kazi kwa juhudi na kuhakikisha huduma katika daraja hilo zinazidi kuboreshwa siku hadi siku na kukidhi matarajio ya Watanzania wote.

Alisema Mfuko uko imara, endelevu na uwekezaji unaendelea kukua kwa kasi hasa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita jambo ambalo limechangiwa na uongozi wa serikali ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Awali, Makamu Mwenyekiti wa PIC, Vuma Augustine, alisema mradi wa daraja hilo una tija kwa taifa kwa sababu ni endelevu na imara na umejengwa kwa viwango vizuri na kuleta faida nyingi zikiwamo za kiuchumi na kijamii.

"Nichukuie nafasi hii kuipongeza serikali kwa uamuzi nzuri wa kujenga daraja hili na pia niipongeze NSSF kwa maamuzi mazuri na ya kizalendo kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja, huu ni uamuzi mzuri kufadhili mradi ambao una tija kubwa kwa jamii na taifa," alisema Augustine.




Mkurugenzi wa Vipindi ITV na Capital TV, Pius Paul (kushoto), akiagana na Mkurugenzi Mkuu wa TCC Plc, Takashi Araki, baada ya wakuu mbalimbali wa vyombo vya habari kufanya ziara katika kiwanda cha TCC ikiwa ni sehemu ya kuendeleza ushirikiano na vyombo vya habari. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## India washerehekea Diwali wakihusisha ziara ya Samia

**Na Romana Mallya**

BALOZI wa India nchini, Binaya Pradhan, amesema kuwa mwaka huu India inasherehekea sikukuu za Diwali, wakizihusisha na ziara ya kihistoria ya India aliyofanya Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni.

Vilevile, amesema katika kukuza uhusiano baina ya nchi hizo kupitia sekta tofauti, mwezi huu wamezindua Taasisi ya Teknolojia ya Madras (IIT) Kampasi ya Zanzibar ambayo itasaidia kueneza maarifa na uvumbuzi kwa vijana wa Tanzania na Afrika.

Balozi Pradhan alibainisha hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati diaspora wa India nchini na wadau wa ndani na nje ya nchi walipoungana nao kusherehekea sikukuu za Diwali.

Sherehe hizo kwa mwaka huu nchini zimefanyika katika Kituo cha Utamaduni wa India Swami Vivekananda (SVCC) kilichoko Masaki jijini.

"Nihitimishe hotuba yangu kwa kusema kwamba Diwali inathamini ustawi, furaha na mafanikio kwa ninyi nyote. Ninawatakia kila mtu heri ya Diwali," alisema.

Kihistoria Diwali ni moja ya sherehe muhimu kwenye eneo la tamasha la India ikijulikana kama 'Sherehe ya Taa', zikimaanisha ushindi na nuru juu ya ujinga.

Sherehe hizi huazimishwa na mikusanyiko ya familia, nguo mpya, chakula maalum na moto wakiamini hufukuza roho mbaya ili kuleta bahati na ustawi katika mwaka mpya wa biashara.

Tarehe za Diwali zinategemea kalenda ya Hindu na mabadiliko kila mwaka, lakini sikukuu hii huangukia kati ya mwezi Oktoba na Desemba.

Wadau wakiwamo viongozi mbalimbali Tanzania na mataifa mengine waliohudhuria walishuhudia ndani ya dakika kadhaa upigaji wa fataki ikiwa ni ishara ya kukamilisha sherehe hizo huku Watanzania wakishiriki kucheza na kuimba nyimbo za utamaduni wa nchi ya India.

Katika sherehe hizo, balozi huyo alitambulisha timu ya wataalamu wa masuala ya Teknolojia ya Habari (TEHAMA) kutoka chuo cha IIT.



# Serikali yawahakikishia viongozi dini kuhubiri hospitalini, magerezani

**Na Jaliwason Jasson,** MBULU

SERIKALI imewahakikishia viongozi wa dini kuwa haitasita kuwaruhusu kutoa huduma za kiroho katika hospitali na magereza ili wananchi waliopo maeneo hayo waweze kuombewa na kupata faraja.

Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara, Kheri James, alitoa hakikisho hilo mwishoni mwa wiki, wakati wa mahafali ya kwanza ya Chuo cha East Africa Theological Institute, Ndaki ya Mbulu (ECLEA-TANZANIA).

Alitoa ahadi hiyo kwa viongozi hao, wakati akijibu risala ya wahitimu 15 wa Stashahada ya Theolojia na Uongozi katika chuo hicho iliyosomwa na Constantine Kifunda.

Aidha, alisema ili waweze kuruhusiwa kwenda kutoa huduma hospitalini na magereza ni lazima wawe na barua ya ithibati kutoka kwa maaskofu wao wakitambulishwa kwa serikali kuwa wao ndio watakuwa wanatoa huduma.

"Tunafanya hivyo kwasababu za kiusalama maana siku hizi kuna uhalifu mwingi na kuna tishio la ugaidi, hivyo kama askofu wako ndiye ameruhusu tunambana anatusaidia kufanya uchunguzi," alisema James.

Pia aliwaelekeza viongozi hao kufuata utaratibu kupitia kwa viongozi wao ili waweze kuruhusiwa kupeleka huduma ya kiroho hospitalini na magereza.

Kuhusu ombi la kupata kiwanja cha kujenga chuo, aliwaelekeza kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, ambao wana viwanja vya kupima na kuuza ili wapewe utaratibu na wakishapewa utaratibu aliahidi kuwaunga mkono.

Katika hatua nyingine mkuu huyo wa wilaya alikemea tabia ya wazazi kuwanyima fursa watoto wa kike kwenda shule.

"Tunapokubali kupokea ng'ombe ili watoto wa kike waolewe tunakosea maana kwa sababu wangesoma wangekuwa wauguzi na kuwasaidia wajawazito wanaoteseka hospitalini kwa kuogopa kuhudumiwa na wauguzi vijana," alisema.

Mkuu wa chuo hicho, Dk. Ibrahim Joramu, alisema masomo wanayofundisha ni uwakili wa kibiblia, uwakili wa fedha na mali, ndoa na usuluhishi, msamaha na upatanisho na theolojia ya biblia.

Askofu Emmanuel Banga wa Kanisa la Mungu, Jimbo la Mbulu, alisema jamii imeathiriwa na utandawazi hivyo aliwataka wahitimu hao kwenda kuifundisha jamii.




Mtafiti wa upimaji udongo na uzalishaji miche bora ya mkonge kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Mlingano, Emanuel Mganda (kulia), akifafanua jambo kuhusu upimaji wa udongo kwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji (wa pili kushoto), alipotembelea banda hilo jijini Tanga mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Mkonge wachangia asilimia 65 akiba fedha za kigeni

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MKURUGENZI Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Saddy Kambona, amesema mkonge unachangia akiba ya fedha za kigeni kwa asilimia 65.

Amesema kutokana na mchango huo, hadi sasa nchi ina fursa nyingi za kuwekeza katika kilimo cha zao hilo.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika Kongamano la Uwekezaji, Biashara na Utalii, Mkoa wa Tanga, lililofunguliwa na Waziri wa Uwekezaji na Mipango, Prof. Kitila Mkumbo, kwa niaba ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Katika kongamano hilo, sekta za umma na binafsi zilipata fursa ya kueleza baadhi ya vikwazo vinavyosababisha kuzorota katika utekelezaji wa majukumu yao ya uzalishaji.

Kwa mujibu wa Kambona, katika kuliongezea mnyororo wa thamani zao hilo, mwaka 2019 serikali iliamua kulifanya zao la kimkakati na kutumia nguvu kubwa kuwahamasisha wakulima wadogo kujikita kwenye uzalishaji wa zao hilo.

"Serikali iliona umuhimu mkubwa sana kuchagiza uzalishaji na kuwashirikisha wakulima wadogo. Mafanikio yaliyopo sasa ni matokeo ya kampeni ya Waziri Mkuu mwenyewe, aliyoizindua Machi, mwaka 2020," alisema.

Katika hatua nyingine, Mkurugenzi wa Masoko wa Mamlaka ya Bandari nchini (TPA), Dk. George Fasha, alisema Bandari ni kiungo muhimu cha kuwezesha uhalisi wa jitihada za serikali na wadau kuingia katika uwekezaji halisi katika Mkoa wa Tanga.

Alisema uzalishaji wa mazao, tija yake katika mauzo nje ya nchini inachagizwa na Bandari, ambayo kiungo kikuu cha uchukuzi katika Ukanda wa Kaskazini mwa Tanzania na nchi jirani.

Alifafanua kuwa serikali kupitia TPA imefanya mradi mkubwa katika Bandari ya Tanga ili kukidhi mahitaji ya wananchi na kufungua fursa za kiuchumi.

Alisema serikali imetekeleza miradi miwili ya maboresho katika bandari hiyo ambapo mradi wa kwanza ni kupanua lango la kutokea na kuingilia bandarini lenye upana wa mita 73.

Alitaja shughuli nyingine ni kuongeza kina cha maji kwa kuchimba kutoka mita tatu za awali hadi kufikia mita 13, kupanua eneo la kugeuzia meli kuwa na kipimo cha mita 800 na ununuzi wa mitambo 16 ya kuhudumia vituo vya mafuta ya magari na mitambo.

"Mradi huu wa awamu ya kwanza umegharimu Sh. bilioni 172.3 ambao umekamilika kwa asilimia 100 na tayari meli kubwa zimeanza kuingia, huku mitambo mipya yenye ufanisi mkubwa ikiwa bandarini, hatua ya sasa ya meli kubwa kutia nanga imeondoa kero ya muda mrefu ya uchukuzi," alisisitiza.

Dk. Fasha, alieleza zaidi kuwa mradi wa awamu ya pili umeiwezesha TPA kufanya maboresho ya gati la zamani kuwa la kisasa likiwa na urefu wa mita 450, kina cha maji 13, yadi ya makasha kontena ya mita za mraba 7,230.

Alisema: "Gati hili lina uwezo wa kuhudumia meli za makasha mawili yenye urefu wa mita 220 pamoja na kubeba hadi tani 60, 000 kwa wakati mmoja, awamu hii ya pili nayo imekamilika kwa asilimia 100 kwa Sh. bilioni 256.8."

# Ujerumani, Korea Kusini zawajengea uwezo vijana 200

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

VIJANA 200 kutoka mikoa ya Arusha, Geita, Simiyu na Manyara, wamejengewa uwezo wa kuchangamkia fursa za ajira katika teknolojia ya nishati ya jua, baada ya Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) kuwajumuisha na kuwapa mwanga kupitia mradi wa E for D.

Mradi huo unafadhiliwa na Serikali ya Ujerumani na Korea Kusini.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya kuhitimisha mradi huo, Ofisa Biashara wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Willfredy Kawa, alisema vijana hao ni miongoni mwa wale wanaokabiliwa na tatizo la ajira.

"Inapoanzishwa miradi ambayo inatoa fursa ya ajira kwa vijana, ni manufaa kwa nchi yetu hasa tunapokumbuka kuwa asilimia 60 ya wananchi wa Tanzania ni vijana na wanakabiliwa na uhaba wa ajira," alisema Kawa.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Nishati Jadidifu Tanzania, Prosper Mwangeli, alisema mradi huo umewajumuisha vijana wa jinsia zote wakiwamo wasichana na vijana wa kiume.

Kaimu Mkuu wa mradi huo, Denis Mbangula, alisema mradi huo ulianza kutekelezwa mwaka 2020 kwa ushirikiano na Ofisi ya Waziri Mkuu (Vijana, Ajira, Kazi na wenye Ulemavu), ukilenga kuwawezesha vijana wa Tanzania kupata ujuzi kwa ajili ya kujiendeleza wenyewe.

Mmoja wa wanufaika wa mafunzo hayo, Said Hamza, aliishukuru GIZ na wafadhili wa mradi huo kwa kutofanya upendeleo kwa baadhi ya vijana.





# Kigwangala aomba madaktari bingwa kuongezewa mshahara

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MBUNGE wa Nzega Vijijini (CCM), Dk. Khamisi Kigwangala, amemwomba Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Honoratha Rutatinisibwa, kuwaongezea malipo ya muda wa ziada madaktari bingwa wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Tabora Kitete, ili waache kukimbilia hospitali za binafsi na kuacha uhitaji hospitalini hapo.

Alitoa ombi hilo juzi alipotembea hospitali hiyo akiwa ameambatana na wadau wa afya kutoka Chama cha Mapambano dhidi ya Malaria, ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya siku mbili katika Hospitali ya Rufani Kitete na Wilaya ya Uyui.

Kigwangala alisema madaktari bingwa wakilipwa fedha za muda wa ziada watafanya kazi kwa jitihada na hawatotumia muda wa ziada kukimbilia hospitali za watu binafsi.

Mbunge huyo alisema katika Hospitali ya Kitete kuna vifaa vingi zaidi kuliko hospitali binafsi, hivyo madaktari hao wanatakiwa kuvitumia ipasavyo kuwahudumia wananchi ili kutimiza adhima ya serikali.

"Yapo majengo yenye hadhi pamoja na vifaa vya kutosha lakini suala la madaktari bingwa kutokufanya kazi katika muda wa ziada na kutumia muda huo katika hospitali binafsi linazidi kuliondolea sifa hospitali zetu, tuwape motisha kwa fedha hizo waisaidie jamii.

"Tunasahau maendeleo yanaletwa na watu syio na majengo kwa sababu serikali ikipata fedha itajenga kila siku, hivyo tuhakikishe wananchi wanapata huduma stahiki," alisema Dk. Kigwangala.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Mark Waziri, alisema hospitalini hapo wanaupungufu wa watumishi 156, madaktari 21 ambapo kwa sasa wapo watatu ambao hawakidhi idadi ya wagonjwa wanaofika hospitalini.

Vilevile alisema upatikanaji wa dawa kutoka juu ni asilimia 57.3 na fedha za miradi ya ndani ni Sh. milioni 800 katika mwaka wa fedha 2023/2024 na mpaka sasa makusanyo yanaendelea vizuri.

Alisema: "Kwa Oktoba makusanyo mapato ya ndani ni Sh.milioni 142 na bima ni Sh.milioni 172 ambapo miradi 15 ya msamaha wa wazee wenye umri wa miaka 60, watu wasiojiweza, watoto chini ya miaka mitano, wajawazito na wagonjwa sugu, waliopata ajali na wafungwa wamehudumiwa kwa gharama ya Sh. milioni 27".




Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, Khamis Katimba, akiwa na Meneja wa Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, Cheick Sangare (katikati), pamoja baadhi ya wanawake waliohudhuria uzinduzi wa kampeni ya kutokomeza malaria inayojulikana kama Zero Malaria Inaanza na Mimi, Wewe na Sisi, Sote uliofanyika eneo la Bugarama wilayani Msalala mkoani Shinyanga mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# M/Kiti Halmashauri aagiza wahujumu maji wakamatwe

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Yanga Makanga, ameagiza wahujumu wa miundombinu ya maji katika halmashauri hiyo ikiwamo kujiunganishia maji kinyemela wakamatwe na kufikishwa mahakamani.

Alitoa agizo ilo juzi kwa Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Sengerema (SEUWASA), Zabrone Bujiku, wakati wa kikao cha robo ya kwanza cha Baraza la Madiwani na kusema ifikapo Novemba 21, wawe wamekamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Alisema hatua hiyo itakuwa fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama hizo ambazo ni kinyume cha sheria na wanaiingizia hasara serikali na kushindwa kufikia malengo ya kutoa huduma stahiki kwa wananchi.

Aidha, aliwataka wananchi kulipa bili kwa wakati na kuwa walinzi kwa miundombinu hiyo ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa dhidi ya watu wanaowahisi kuhujumu maji hayo.Awali, akitoa taarifa ya utolewaji wa huduma ya maji wilayani hapa, Meneja wa SEUWASA, Zabrone Bujiku alisema kuna watu ambao wamejiunganishia maji kinyemela na kuomba kibali cha kuwachukulia sheria wote waliohusika na wizi huo.

Alisema wizi huo unasababisha mamlaka kushindwa kujiendesha.

Baadhi ya madiwani wa halmashauri hiyo, akiwamo Diwani wa Kata ya Chifufu, Robarth Madaha alisema wote waliojiunganishia maji kihuni wanatakiwa kufikishwa katika vyombo husika.

## TAKUKURU yatembelea kata saba, yapokea malalamiko 62

**Na Jenesta Jasson,** KAGERA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kagera imetembelea kata saba katika kipindi cha miezi mitatu na kupata malalamiko 62 ya vitendo vya rushwa pamoja na ukiukwaji wa haki za wananchi.

Hayo yamebainishwa na Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Kagera, Ezikia Sinkala, wakati akiwasilisha kwa waandishi wa habari taarifa ya utendaji kazi wa taasisi hiyo katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Julai hadi Septemba 2023.

Sinkala alisema kati ya malalamiko hayo waliyoyapokea 36 hayakuhusiana moja kwa moja na rushwa, huku 36 yalihusiana na rushwa, ambapo 18 tayari yamechukuliwa hatua na 18 yanaendelea kufanyiwa uchunguzi ili kufikishwa katika vyombo vya kisheria.

Vilevile alisema taasisi hiyo ilifanya uchambuzi wa mifumo ya taasisi za serikali na sekta binafsi katika ukataji na ukusanyaji wa kodi ya zuio ili kuhakikisha kodi zinawasilishwa katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kuondoa mianya ya rushwa.

Alisema katika uchambuzi huo walibaini upungufu kutokana na ukataji wa kodi ya zuio kutozingatia viwango vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria.

Sinkala alisema baada ya kubaini upungufu huo kilifanyika kikao cha kuhimiza taasisi zote za serikali na sekta binafsi kuhakikisha wanarejesha fedha hizo za kodi katika mamlaka husika ambazo zimeisababishia serikali hasara.

Aidha, aliwataka watumishi wa umma na sekta binafsi na wananchi kuzingatia sheria za makato ya mfumo wa ukusanyaji kodi, huku akiitaka serikali kutimiza majukumu yake na kuwa makini na fedha zinazotokana na makusanyo ya kodi na vyanzo vingine kwa kuzingatia sheria na kanuni za ukusanyaji mapato.

Baadhi ya wananchi mkoani hapa wakiwamo waliofikiwa na elimu ya kuripoti matukio ya rushwa na kuwasilisha kero zao waliiomba serikali kuweka mkakati madhubuti utakaosaidia kudhibiti vitendo vya rushwa hususani katika maeneo muhimu ya huduma za jamii.

Nipashe

# Spotika



SABABU 5 LIVERPOOL KUWA NA WASIWASI MSIMU HUU UK. 12-13



SANE

# WASHAMBULIAJI WA5 BORA ULAYA KWA SASA

## ISIKUPITE

UFARANSA imejiwekea rekodi yake ya kipigo kikubwa zaidi kuwahi kukitoa wakati ikifunga mabao saba kila kipindi kwenye ushindi wa 14-0 dhidi ya Gibraltar, mchezo wa kuwania kufuzu Euro 2024, huku Kylian Mbappe mbali ya kuhusika katika mabao matano aliondoka na mpira baada ya kupiga hat-trick na asisti mbili. Mabao mengine yalifungwa na Ethan Santos (kujifunga), Marcus Thuram, Warren Zaire-Emery, Jonathan Clauss, Youssouf Fofana, Adrien Rabiot, Ousmane Dembele na Olivier Giroud (mawili).



**LONDON,** England

LIGI tano bora za Ulaya, yaani Ligi Kuu England, LaLiga (Hispania), Serie A (Italia), Bundesliga (Ujerumani) na Ligue 1 (Ufaransa), kwa pamoja zinaunda kilele cha mashindano ya soka barani humo.

Ligi hizi zinaonesha kiwango cha juu cha vipaji, ubora wa mbinu na ushindani mkubwa. Vita vikali vinavyoshuhudiwa katika ligi hizi ni chimbuko la baadhi ya vipaji vya kipekee vya soka kutoka duniani kote.

Wachezaji wanaofanya vizuri katika mazingira haya yenye ushindani mkubwa mara nyingi huchukuliwa kuwa bora zaidi kwenye sayari hii, kwani ujuzi wao hujaribiwa kila mara na kuboreshwa dhidi ya upinzani mkali zaidi.

Bila kuchelewa, hebu tuangalie wachezaji watano bora zaidi kulingana na ukadiriaji wa Ulaya hadi sasa msimu huu wa 2023-24...

**#5 Kylian Mbappe (Paris Saint-Germain) - 8.03**

Huku Lionel Messi na Neymar wakimaliza ushirika wao na Paris Saint-Germain na kuhama msimu wa majira ya joto, Kylian Mbappe kwa mara nyingine amekuwa mtu mkuu katika klabu hiyo. Mfaransa huyo amekuwa mchezaji wao bora kwa miaka kadhaa sasa na ameonesha uwezo wake wa ajabu wa kufunga tena msimu huu.

Mbappe amekuwa katika fomu ya juu kwa miamba hao wa Jiji la Paris katika hatua za mwanzo za msimu mpya. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amefunga mabao 13 na kutoa asisti moja katika mechi 11 za Ligue 1 akiwa na PSG hadi sasa msimu huu.

Amekuwa katika hali nzuri sana hivi karibuni, akifunga mabao sita na kutoa asisti katika mechi zake nne zilizopita za Ligue 1.

**#4 Jude Bellingham (Real Madrid) - 8.04**

Je, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 20, ametulia vema katika Klabu ya Real Madrid, mojawapo ya klabu kubwa zaidi duniani. Amekuwa mbunifu mkuu nyuma ya mafanikio yao katika hatua za mwanzo za msimu wa 2023-24.

Akicheza katika nafasi ya juu zaidi kuliko kawaida, Bellingham amekuwa kituo kikuu cha mabao kwa upande wa kocha Carlo Ancelotti hadi sasa msimu huu. Si tu kwamba amekuwa muhimu kwa mabao yake, lakini Bellingham pia amekuwa na sifa zake za uongozi na uwezo wa kuibuka wakati muhimu.

Amefunga mabao 10 na kutoa asisti mbili katika mechi 11 za LaLiga akiwa na Real Madrid hadi sasa. Bellingham ametwaa tuzo tano za mchezaji bora wa mechi pia.

**#3 Harry Kane (Bayern Munich) - 8.36**

Harry Kane alijiunga na Bayern Munich msimu huu wa majira ya joto ili kumaliza msururu wake wa kutotwaa ubingwa mwishoni mwa msimu huu. Amekuwa akifanya yake kuelekea jambo hilo kwa mtindo wa kuvutia.

Hakujawa na shaka yoyote juu ya ubora wa Kane kama mshambuliaji wa kati, lakini namba anazoweka kwenye Bundesliga ni za kutisha. Kane ameanza maisha ya kuvutia huko Bavaria.

Baada ya mechi 11 pekee za ligi, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, tayari amevuka idadi ya mabao ya mshindi wa Kiatu cha Dhahabu cha Bundesliga msimu uliopita, Niclas Fullkrug (16). Mwingereza huyo tayari amefunga mabao 17 na kutoa asisti tano katika mechi 11 za Bundesliga hadi sasa msimu huu.

**#2 Serhou Guirassy (Vfb Stuttgart) - 8.40**

Bado mshambuliaji mwingine ambaye haonekani kuacha kufunga katika Bundesliga ni mchezaji wa Kimataifa wa Guinea, Serhou Guirassy. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, amekuwa katika kiwango cha kustaajabisha cha kufunga mabao katika Klabu ya VfB Stuttgart hadi sasa msimu huu.

Ni fowadi aliyekamilika ambaye uwezo wake wa kucheza nafasi ya kiungo na upigaji mashuti umekuwa wa kipekee katika msimu mpya. Vitendo vya Guirassy vimechangia pakubwa katika msimu wa mapema wa VfB Stuttgart ambao unawafanya kushika nafasi ya tatu kwenye jedwali la Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Katika mechi tisa kwenye michuano yote hadi sasa msimu huu, Guirassy amefunga mabao 15 na kutoa asisti moja.

**#1 Leroy Sane (Bayern Munich) - 8.53**

Uchezaji mzuri wa fowadi Leroy Sane umeifanya Bayern Munich kuwa na nguvu isiyoweza kuzuilika ndani ya safu ya tatu ya ushambuliaji katika robo ya kwanza ya msimu mpya. Sane amekuwa katika kiwango bora, akifunga mabao na kutengeneza nafasi kwa wachezaji wenzake kutokana na sifa zake za kiufundi na maono.

Sane amekuwa zaidi ya wachezaji wachache kukabiliana na wapinzani kwani amekuwa akiwakimbia kwa kasi, ustadi wa kucheza chenga na wepesi. Kwa sasa ndiye mchezaji aliye na viwango vya juu zaidi katika ligi tano bora za Ulaya akiwa na wastani wa 8.53 katika Bundesliga.

Katika mechi 11 za ligi hadi sasa msimu huu, Mjerumani huyo amefunga mabao manane na kutoa asisti sita.

Extra Time

# SABABU TANO LIVERPOOL KUWA NA WASIWASI MSIMU HUU



**LIVERPOOL,** England

MSIMU wa kusikitisha wa 2022-23 ulichochea mabadiliko katika msimu wa majira ya joto pale Liverpool. Jurgen Klopp huenda hakupata wachezaji haswa aliowataka lakini 'Wekundu' hao walifanya biashara nzuri wakati huo wa dirisha la usajili.

**Pamoja na vipaji ambavyo tayari vipo kwenye orodha ya malipo, ilionekana kuwa Liverpool walikuwa na kile wanachohitaji kufufua bahati yao.**

Mambo yamekuwa ya kupendeza katika hatua za mwanzo za msimu wa 2023-24. Lakini kuna hisia kwamba wameweza kuweka karatasi juu ya nyufa.

Kipigo cha mabao 3-2 kutoka kwa Toulouse kwenye Ligi ya Europa Novemba 9, mwaka huu kilifichua baadhi ya udhaifu wao.

Liverpool ilionekana kama timu isiyo na muunganiko katika muda wote wa mchezo. Kuna masuala machache ambayo Klopp anatakiwa kuyashughulikia kabla, ili timu hii ya Liverpool iweze kurudi kwenye mtindo wao wa zamani.

Makala haya inaangalia sababu tano kwa nini Liverpool inahitaji kuwa na wasiwasi msimu huu, twende sasa...

### #5 Ulinzi bado unavujisha mabao

Liverpool ilikuwa moja ya timu zenye ulinzi mkali zaidi barani Ulaya wakati wa miaka yao bora chini ya Klopp. Licha ya matokeo yao ya kutia moyo hadi sasa katika msimu huu wa 2023-24, 'Wekundu' hao hawajaweza kuzuia mpira nje ya lango lao.

Kufungwa mabao matatu dhidi ya Toulouse, mpinzani wao wa Ligi ya Europa, ni jambo linalomtia wasiwasi Klopp kwa sasa. Huku Virgil van Dijk akikosekana, kuna ukosefu wa uongozi wa nyuma ambao Liverpool wanaonekana kuumia.

Wameruhusu mabao 15 katika mechi 15 kwenye Ligi Kuu na Ligi ya Europa hadi sasa msimu huu. Hilo linahitaji kubadilika ikiwa Liverpool wanataka kushinda tuzo za juu.

Wamefanikiwa kucheza mechi moja pekee bila kuruhusu bao katika mechi zao tano zilizopita kwenye mashindano yote.

### #4 Ukosefu wa mabeki bora wa pembeni

Haikuwa muda mrefu sana ambapo Kostas Tsimikas alitazamwa kama mojawapo ya beki bora wa kushoto kwenye Ligi Kuu. Lakini kiwango chake cha uchezaji kimeshuka sana na yeye si msaidizi mzuri wa Andy Robertson.

Huku Robertson sasa akiwa ameondolewa hadi mwisho wa mwaka, Klopp anatakiwa ama kumpata Tsimikas ili kuimarika au kusajili beki mwingine wa kushoto. Hakuna mrithi sahihi wa Trent Alexander-Arnold pia. Muingereza huyo anacheza nafasi ya juu sana siku hizi, lakini Joe Gomez, ambaye anaziba nafasi yake, kimsingi ni beki wa kati.

Wakati wa miaka bora ya Liverpool chini ya Klopp, Liverpool walikuwa wakitegemea sana mabeki wao wa pembeni kama vituo vya ubunifu. Hata leo, wakati mabeki wao wa pembeni wanapokuwa chini ya kiwango, Liverpool wanaelekea kuporomoka.

### #3 Alexis Mac Allister bado hajaimarika

Alexis Mac Allister ametumia muda mwingi wa siku zake za awali akiwa Liverpool akicheza kama kiungo mkabaji. Amejitahidi kujiimarisha kwenye safu ya kiungo ya Wekundu hao na inatakiwa kusemwa kuwa si nafasi yake anayopendelea.

Amejitahidi kukabiliana na mabadiliko ya ulinzi na anaonekana kuchelewa kwa sekunde moja au mbili kwa changamoto mara kwa mara. Hii imemfanya achukue kadi tano za katika mechi 11 za Ligi Kuu. Kwa matokeo hayo, Mac Allister amefungiwa kucheza mchezo unaofuata dhidi ya Brentford.

Mac Allister anafanya kazi vema zaidi katika jukumu la hali ya juu zaidi ambapo ujuzi wake wa kuendeleza mpira na uwezo wa kutengeneza pasi ngumu kunaweza kusaidia Liverpool kuharibu safu ya ulinzi.

Chaguo jingine ambalo Liverpool wanalo kwenye safu ya kiungo ya ulinzi ni Wataru Endo na hayuko kwenye daraja sawa na Fabinho ambaye alikuwa kiini cha mafanikio ya Liverpool chini ya Klopp.

### #2 Uwezo mdogo wa mashambulizi ya kushtukiza

Chapa ya 'chuma kizito' ya Klopp ya soka ina sifa ya ukandamizaji mkali wa kupiga mashuti. Kila wakati Liverpool inapopoteza mpira, wachezaji wao hukusanyika kwa nguvu ili kuupata tena. Aina hii ya mabadiliko ya ulinzi yenye kuleta uwezo wa kudumisha kiwango cha juu wakati wa michezo ndiyo iliyoitofautisha Liverpool hapo awali.

Mashambulizi ya kushtukiza ya Liverpool hayajafanyika vizuri haswa wakati wa wiki ya mchezo wa Ulaya.

Iwapo orodha ya sasa haiwezi kukidhi matakwa ya mpango wa mchezo unaoshindanisha, Klopp anaweza hata kulazimika kubuni mbinu mpya.

### #1 Kiwango duni ugenini

Kiwango cha Liverpool ugenini kimeshukiwa hadi sasa msimu huu. 'Wekundu' hao wamepata ushindi mmoja pekee katika mechi zao tano zilizopita za ugenini katika michuano yote.

Walilazimishwa sare ya bao 1-1 na Chelsea kwenye Uwanja wa Stamford Bridge katika mechi yao ya kwanza ya Ligi Kuu England. Wameshindwa pia na Tottenham Hotspur na kutoka sare na Brighton & Hove Albion. Sare na Luton Town katika Uwanja wa Kenilworth Road na kupoteza kwa mabao 3-2 Alhamisi usiku dhidi ya Toulouse ugenini.

Kabla ya kuivaa Toulouse Liverpool ilishinda mabao 5-1 kwenye Uwanja wa Anfield wiki chache zilizopita. Kuanguka kwa kupoteza 3-2 kwao labda kunaonesha shida ya mtazamo wao ugenini.

## Nukuu

"Cristiano [Ronaldo] ni mchezaji mkubwa, lakini wale wanaosema yeye ni bora kuliko Messi [Lionel] hawajui lolote kuhusu soka, au wanasema kwa nia mbaya. Messi ni mmoja wa aina yake. Haiwezekani kuiga na haiwezekani kurudia. Mchezaji kama yeye huja kila baada ya miaka 50 au 100," **Mshambulizi wa zamani wa Ajax na AC Milan, Marco van Basten**



"Pamoja na Ufaransa, Kylian Mbappe, angekuwa na nafasi nzuri pia, na nani anajua? Anacheza katika timu ambayo ina nafasi kubwa ya kushinda Ligi ya Mabingwa pia, lakini kati ya majina hayo manne bora hivi sasa, nadhani ingekuwa hivyo itakuwa ngumu sana kwa Haaland kushinda kwa sababu ya nchi anayochezea. Isipokuwa labda Manchester City watwae tena makombe matatu kwa msimu, au ashangaze tena kwenye Ligi ya Mabingwa. Wachezaji wengine ambao nimewataja hivi punde labda wamepata fursa nyingine na mashindano katika majira ya joto," **Nyota wa zamani wa Liverpool na mchambuzi wa soka, Jamie Carragher akiwataja taja Jude Bellingham, Harry Kane, Kylian Mbappe na Erling Haaland kuwa mmojawapo anaweza kutwa Tuzo ya Ballon d'Or 2024.**



"Nilipokuwa Paris, sikuwa navaa jezi namba 10. Tangu miaka hiyo nilipochezea timu ya taifa nikiwa Barcelona, nilizoea kuvaa jezi namba 10 kila mara."Ijapokuwa sio jambo kubwa, niliikosa sana jezi namba 10 zaidi nilipokuwa PSG, kwa sababu niliizoea. Na hiyo ndio maana ya namba 30. Nilianza kucheza na namba 30, mechi yangu ya kwanza ilikuwa na namba 30, kwa hivyo kuna kitu maalum kwa hilo kwangu pia," **Mshambuliaji wa Inter Miami, Lionel Messi, katika mahojiano na Zinedine Zidane, yaliyodhaminiwa na Adidas.**





ROBERTINHO

# RAUNDI TISA LIGI KUU BARA ZILIVYOFUTA KAZI MAKOCHA SABA

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA ni raundi ya tisa tu ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/24, tayari makocha saba wameshaziacha timu walizokuwa wakizifundisha kutokana na sababu mbalimbali kama vile kufukuzwa, kuondoka wenyewe, kujizulu na mengine yanayofanana na hayo.

**Roberto Oliveira wa Simba amekuwa kocha wa saba kuachana na timu za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.**

Vyovyote iwavyo, sababu kubwa za makocha wote ni kutokana na kufanya vibaya kwa timu walizokuwa wakizifundisha.

Hii ni idadi kubwa zaidi kuwahi kutokea kwa raundi chache hizi. Haijulikani mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza ni makocha wangapi watakuwa wameshaondoka, au kuoneshwa mlango wa kutokea kwenye klabu zao.

Wakati makala haya ikichambua makocha hao kufutwa kazi, bado kuna fukuto linaloendelea kwenye Klabu ya Geita Gold, na huenda lolote linaweza kutokea kwa Kocha Hemed Suleiman 'Morocco' naye kuungana na hao saba.

Makala haya imekusanya makocha wote walioondoka kwenye klabu wanazofundisha na sababu zilizowafanya 'ndoa' zao na klabu hizo kuvunjwa, twende sasa...

### Hans Van Pluijm - Singida FG

Katikati ya Septemba tu, Kocha Mkuu wa Singida Fountain Gate, Mholanzi Hans Van der Pluijm, alitangaza kujiuzulu kuifundisha timu hiyo mara tu baada ya kufanikiwa kuivusha kwa tabu hatua ya Raundi ya Kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya JKU ya Zanzibar.

Pluijm alijiuzulu kwa kile alichoeleza kuwa anahitaji muda zaidi kwa ajili ya masuala yake binafsi.

Katika mechi ya kwanza ya hatua za awali, Agosti 18, aliiongoza timu hiyo kushinda mabao 4-1, na mechi ya marudiano kwenye uwanja huo huo wa Azam Complex, Agosti 27, ilichapwa mabao 2-0, lakini ikafanikiwa kusonga mbele kwa jumla ya mabao 4-3.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo, zilieleza wakubwa hawakufurahishwa na kiwango kilichooneshwa na timu hiyo katika mechi ya pili, na ilikuwa haijafanya vema kwenye mechi za Ngao ya Jamii, hivyo kwa heshima yake wakamtaka aandike mwenye barua ya kujiuzulu.

### Ernest Middendorp - Singida FG

Singida Fontaine Gate ndiyo timu inayoongozwa kwa kuachana na makocha wawili kwa msimu mmoja mpaka sasa.

Tena wote wameondoka kwa vipindi visivyotofautiana sana. Mjerumani huyu ndiye aliyerithi mikoba ya Hans van der Pluijm.

Alihudumu kwenye timu hiyo kwa muda wa wiki mbili tu, akiiongoza katika mechi moja tu ya hatua ya Raundi ya Kwanza, Kombe la Shirikisho dhidi ya Future FC ya Misri na kushinda bao 1-0.

Middendorp aliondoka ghafla baada ya mechi hiyo, na akanukuliwa kwenye baadhi ya vyombo vya habari kuwa ameondoka kwa sababu hataki kupangiwa kikosi na baadhi ya viongozi wa timu hiyo.

### Zuberi Katwila - Ihefu

Ushindi wake pekee ulikuwa ni kuifunga Yanga mabao 2-1 kwenye mchezo uliochezwa Oktoba 4, mwaka huu.

Kabla ya hapo na baada, Ihefu ilikuwa na mwenendo wa kusuasua hadi pale ilipotoka taarifa ya Ihefu na kocha huyo kuachana kwa makubaliano ya pande mbili.

Na hili lilifanyika baada ya Ihefu kufungwa bao 1-0 dhidi ya KMC Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Oktoba 7, mwaka huu.

Hata hivyo, kulikuwa na fununu kuwa Katwila alikuwa anatakiwa na Mtibwa ambayo nayo ilikuwa hoi bin taaban na ilikuwa inataka kumfungashia virago kocha wake, Habib Kondo.

Na kweli baadaye ikawa hivyo, Katwila anaweka rekodi ya kuwa kocha pekee kati ya wote hawa walioondoka timu moja na kwenda kuifundisha tena timu nyingine ya Ligi Kuu.

### Habib Kondo - Mtibwa Sugar

Mara baada ya kupokea kipigo cha mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Manungu, Turiani, Morogoro, Klabu ya Mtibwa Sugar ikatangaza kuachana na kocha wake, Habib Kondo, kutokana na mfululizo wa matokeo mabovu.

Mechi hiyo ilichezwa Oktoba 19, na mpaka wakati huo ilikuwa haijaonja ladha yoyote ya ushindi ikicheza mechi tano, ikipoteza tatu na kutoa sare mbili tu, matokeo ambayo yalitosha kumwondoa kwenye orodha ya walimu kwenye Ligi Kuu na Katwila akachukua nafasi yake.

### Cedric Kaze - Namungo

Alijinyoa mwenyewe kabla hajanyolewa. Ilikuwa ni Oktoba 22, mwaka huu alipoandika barua ya kujiuzulu kutokana na matokeo mabaya ya timu yake ya Namungo FC.

Hakuwa na matokeo mazuri aliyopata kwani katika mechi sita alizocheza mwanzo hakuna hata moja aliyoshinda.

"Leo nimetangaza kung'atuka kwenye nafasi ya kuwa Kocha Mkuu wa Namungo, ningependa kutumia fursa hii kuushukuru uongozi na watendaji wenzangu wa benchi la ufundi na wachezaji kwa ushirikiano na kujitoa kwao," aliandika kocha huyo.

### Mwinyi Zahera - Coastal Union

Katikati ya Oktoba, Klabu ya Coastal Union ilitumia staili ya aina yake kumwondoa Kocha Mkuu Mwinyi Zahera kwenye nafasi yake ya kuwa kocha mkuu na kumpeleka kuwa Mkurungenzi wa Ufundi.

Hii ni baada ya Coasta Union kuanza vibaya mechi zake za Ligi Kuu na hadi anaondolewa kwenye nafasi hiyo, ilikuwa haijashinda mechi yoyote.

Baada ya kuondolewa, ilibaki na Kocha Msaidizi, Fikirini Elias, ambaye angalau alianza kufanya vema, kabla ya kumpata Kocha Mkuu mpya, David Ouma.

### Roberto Oliveira - Simba

Alitimuliwa baada ya timu ya Simba kubugizwa mabao 5-1 na watani wao wa jadi, Yanga, Novemba 5, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. Kabla ya hapo alikuwa na rekodi nzuri kuliko kocha yeyote wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Tangu alipotimuliwa hadi leo Simba haijapata Kocha Mkuu, na huenda ikacheza mechi ya Jumamosi dhidi ya Asec Mimosas ikiwa chini ya Kaimu, Daniel Cadena, akisaidiana na Selemani Matola.

## JE, WAJUA?



MASTAA wakubwa watano ambao wameonesha kiwango duni Ligi Kuu England msimu huu; #5 Alexis Mac Allister (Liverpool), #4 Kai Havertz (Arsenal), #3 Moises Caicedo (Chelsea), #2 Casemiro (Manchester United) na #1 Marcus Rashford (Manchester United).



HABARI DODOMA

# Serikali yaifutia leseni kampuni, yawapa wachimbaji

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WIZARA ya Madini imetangaza kufuta leseni ya utafiti uliokuwa unafanywa na Kampuni ya Sekenke Exploration Limited katika eneo la mgodi wa Sekenke One uliopo Wilaya ya Iramba mkoani hapa.

Hivyo, wachimbaji wadogo watapewa leseni zaidi ya 300 kwa ajili ya kuanza shughuli za uchimbaji wa madini katika mgodi huo.

Kufutwa kwa leseni ya kampuni hiyo ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu alilolitoa Oktoba 17, 2023 alipofanya ziara mkoani hapa.

Pamoja na mambo mengine, Rais Samia aliiagiza Wizara ya Madini kuangalia taratibu za kisheria ambazo zitawezesha wachimbaji wadogo kupewa eneo hilo kufuatia ombi lililotolewa na Mbunge wa Iramba Magharibi, Dk. Mwigulu Nchemba.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde akitangaza kufutwa kwa leseni hiyo juzi wakati akizungumza na wananchi alisema Kampuni ya Sekenke One Mining Limited ilipewa leseni namba 6503 ya mwaka 2010 na ilipofika 2018 leseni hiyo iliisha muda wake wa matumizi.

Alisema kwa mujibu wa Sheria ya Madini Kifungu cha 32 'B' Sura ya 123 ni kwamba leseni ikirejeshwa serikalini sheria inampa mamlaka Waziri wa Madini kupitia Kifungu cha 15 cha Sheria ya Madini kufanya matumizi mengine ya eneo husika.

"Baada ya maelekezo ya Rais kwa heshima naomba nitamke leo Novemba 18, 2023 siku ya Jumamosi Rais ameridhia niwakabidhi leseni za uchimbaji katika eneo la Sekenke One, kwa hiyo kilio chenu cha miaka 10 kimepatiwa majibu," alisema Mavunde huku mamia ya wachimbaji wakishangilia maamuzi hayo.

Mavunde aliwataka wachimbaji watakapopewa leseni hizo wazifanyie kazi zisiwe mapambo ili kusaidia kuinua uchumi wa Wilaya ya Iramba, Mkoa wa Singida na kubadilisha maisha yao wenyewe kutoka hatua moja kwenda hatua mbili mbele.

Naye Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini Tanzania, Mhandisi Yahya Samamba, alisema eneo la mgodi wa Sekenke One lina uwezo wa kutoa leseni za wachimbaji zaidi ya 300 na kwamba hadi sasa tume hiyo imepokea maombi 88 ambapo kati ya hayo 28 ndiyo yametimiza vigezo.

Naye Mbunge wa Iramba Magharibi, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema wachimba ambao wamepeleka maombi lakini wamekosa vigezo kutokana na kushindwa kulipia gharama atawasaidia kuwalipia ili waendelee na shughuli za uchimbaji.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema mkoa huu ulipewa lengo la kukusanya Sh.bilioni 12 katika maduhuli kwa mwaka huu wa fedha lakini hadi sasa zimekusanywa zaidi ya Sh.bilioni sita.




Mshindi wa Sh. milioni 10 kupitia kampeni ya Vodacom Tanzania PLC inayoendelea ya 'Sambaza Shangwe, Gusa Maisha', Maduhu Sayi Msekwa (kulia), akiwa ameshikilia mfano wa hundi aliyokabidhiwa na Masta Shangwe katika viwanja vya Machinga Complex jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Kupitia kampeni hii wateja wanaweza kushinda zawadi mbalimbali ikiwamo bodaboda, runinga, simu za mkononi, router za 4G na 5G pamoja pesa taslimu kila wiki kuanzia shilingi laki tano mpaka milioni 10 kwa kununua vifurushi, kufanya malipo kwa M-Pesa na kupakua DJ Mixes kupitia Mdundo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CBE, SIDO kuendeleza ubunifu wa wanafunzi vyuo vikuu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE) kwa kushirikiana na Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo nchini (SIDO) kimeanzisha programu atamizi za biashara kwa ajili ya kulea na kuendeleza ubunifu mbalimbali zinazondaliwa na wanachuo.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Edda Lwoga, aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye kongamano la wanataaluma ikiwa ni sehemu ya kuelekea mahafali ya 58 ya chuo hicho.

Alisema hadi sasa tayari vijana 185 wamesajiliwa na wanalelewa na chuo hicho na tayari wameshasajili biashara zao BRELA.

Alisema lengo la programu hiyo ni kuwezesha wanachuo kuanza kufanya biashara tangu wakiwa chuoni ili baadaye ubunifu wao uwe biashara kubwa.

Aidha, alisema chuo kimeingia makubaliano na Shirika la Viwango nchini (TBS), Wakala wa Vipimo (WMA) na Serikali Mtandao (e-GA) ili kutoa fursa za wanafunzi wa chuo hicho kujifunza kwa vitendo na kuwapunguzia shida kwenye soko la ajira.

Kadhalika, alisema chuo hicho kinaendelea na jitihada za kusomesha watumishi wake hasa walimu ndani na nje ya nchi ili kuongeza maarifa kulingana na mahitaji ya soko la ajira duniani.

# Wazazi wapewa mbinu kudhibiti ukatili dhidi ya watoto

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeitaka jamii kujenga utaratibu wa kukaa karibu na watoto ili kuwasikiliza na kubaini vitendo vya ukatili wa kijinsia wanavyokumbana navyo.

Ofisa Utamaduni wa Jiji la Dodoma, Ezdori Kuzenza, alitoa rai hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya, Jabir Shekimweri kwenye bonanza la afya ya uzazi lililoandaliwa na Shirika la World Vision lenye lengo la kupinga ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto lililofanyika katika viwanja vya Shule ya Msingi Chang'ombe jijini hapa.

Kuzenza alisema masuala ya kupinga ukatili yanapaswa kuanzia nyumbani kwa wazazi na walezi, ili kuisaidia serikali kubaini wahalifu wanaohusika na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto.

Aliipongeza World Vision kupitia mradi wake wa 'ahadi' unaotekelezwa mkoani Dodoma ambao unalenga kupinga masuala ya ukatili wa kijinsia lakini pia kukuza ndoto za vijana ambao utasaidia kushawishi vijana kufikia malengo yao.

Naye Meneja wa Kanda ya Kati wa World Vision, Pudensiana Rwezaura, alisema bonanza hilo ni kwa ajili ya kuadhimisha siku 10 za kupinga ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na jamii kwa ujumla.

Alisema shirika hilo limeamua kuandaa bonanza hilo ili kuwakumbusha wazazi, kwamba watoto na vijana wanapaswa kuskilizwa ili kuweza kutimiza ndoto zao.

Alifafanua kuwa katika hizo siku za maadhimisho ya kupinga ukatili wa kijinsia kupitia mradi wa ahadi unaotekelezwa mkoani hapa, watakuwa wakifanya vitu mbalimbali ambavyo vitaisaidia jamii kukumbuka kutokomeza ukatili ambao hautakiwi katika jamii.

# Wanafunzi wa Tanzania wang'ara somo la Kichina

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Elimu ya Juu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Peter Msofe, amesema mchango wa maendeleo unaotolewa na China hapa nchini unaleta tija na kuzidisha uhusiano mzuri uliopo wa muda mrefu.

Amesema uhusiano huo umesababisha nchi hizo kushirikiana katika mambo mbalimbali ikiwamo sekta ya elimu, afya na biashara.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa utoaji tuzo kwa wanafunzi wa Tanzania waliofanya vizuri somo la lugha ya kichina.

Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, alisema tangu kuanzishwa kwa tuzo hiyo mwaka 2018 wanafunzi wengi kutoka Tanzania wamesoma lugha hiyo.

Alisema idadi kubwa ya shule zimeanzisha somo la lugha ya kachina na kozi mbalimbali zinaendeleo kufundishwa.

Alisema: "Shauku ya kujifunza lugha ya kichina ilichochewa na mfumo wa elimu Tanzania ambao umeonesha kuungwa mkono na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia".

Alisema kuna wanafunzi 125 wanaojifunza lugha hiyo nchini Tanzania na walimu saba kutoka shule 18 wanaofundisha lugha hiyo walioshinda tuzo ya Balozi wa China mwaka huu.

Mmoja wa wanafunzi waliopata tuzo hiyo kutoka Shule ya Sekondari Zanaki, Gloria Hamphrey alisema alianza kujifunza lugha hiyo akiwa kidato cha kwanza.

# RC atoa onyo kwa madalali wanaonunua maparachichi

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

SERIKALI mkoani Mbeya imeewaonya madalali wanaonunua maparachichi ya wakulima wilayani Rungwe kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria kwa sababu wanaharibu soko la zao hilo kwa kushusha bei ili wapate faida.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa tahadhari hiyo wakati wa kikao cha wadau wa kilimo cha matunda hayo wilayani Rungwe ambapo alizitaka kampuni zinazofanya biashara hiyo kwenda moja kwa moja kwa wakulima.

Alisema kampuni yoyote inayotaka kutumia madalali inatakiwa kuwapatia ajira za muda na kuwapatia vitambulisho maalumu ambavyo vitakuwa vinawatambulisha kama wafanyakazi wake badala ya wao kujiingilia kiholela kwa wakulima.

"Mnunuzi anayenunua maparachichi kwenye maeneo yetu, anatakiwa kuandika barua ya kumtambulisha mwakilishi wake kwa serikali ili atambuliwe na tutakuwa wakali maana tumebaini hawa madalali kuwa chanzo cha kuharibika kwa soko," alisema Homera.

Aliwataka pia wanunuzi hao kununua maparachichi hayo kwa bei elekezi ya Sh. 1,720 kwa kilo na sio chini ya hapo na kwamba atakayekamatwa anakiuka atashughulikiwa.

Hata hivyo aliwataka wanunuzi kuhakikisha wanalipa tozo zote za serikali kabla ya kusafirisha maparachichi na kuyapeleka nje ya wilaya hiyo ikiwamo ushuru na tozo ya Sh. 20 ambayo ni kwa ajili ya maendeleo.

Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Suma Fyandomo, alisema madalali wamekuwa wakiharibu mfumo wa soko la maparachichi kwa kununua yakiwa mabichi jambo ambalo linawasababishia hasara wakulima.

Alisema wakulima wamekuwa wakitumia rasilimali nyingi kuhudumia zao hilo ikiwamo ununuzi wa mbolea lakini madalali wanaponunua matunda yakiwa hayajakomaa wanahujumu soko la zao hilo.

Alisema, baadhi ya madalali hao wamekuwa wakichezea mizani ya kununulia matunda hayo na hivyo kuwanyonya wakulima, tunamshukuru Mkuu wa Mkoa kwa kuliona hili na kukemea, tutaendelea kumuunga mkono."

Hivyo, aliwaomba wadau mbalimbali kuiunga mkono serikali ili kuwakomesha madalali.

# Madiwani watakiwa kutoa elimu athari mvua ya El-Nino

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya, mkoani Mbeya, imewataka madiwani wilayani hapo kushirikiana na watendaji wa serikali kutoa elimu kwa wananchi kuhusu tahadhari wanazopaswa kuchukua ili kuepuka madhara ya mvua ya El-Nino.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye kikao maalumu na madiwani pamoja na watendaji wa halmashauri hiyo.

Alisema madiwani wanayo nguvu kubwa ya kusikilizwa na wananchi kwenye maeneo yao, hivyo ni muhimu wakati watendaji wa serikali wakitoa elimu ya tahadhari zinazopaswa kuchukuliwa na wao wakashiriki. Aliitaja Wilaya ya Chunya kuwa miongoni mwa maeneo yaliyo na wakazi wanaoishi au kufanya shughuli zao kwenye maeneo ya mabonde, hivyo TMA inapotabiri kuwepo kwa mvua nyingi lazima tahadhari izingatiwe na watu wote.

"Tumeshatangaziwa msimu huu tunaweza kuwa na mvua za wastani au zitakazokuwa juu ya wastani kwenye baadhi ya maeneo na kuna maeneo yawezekana kukawa na El-nino, sasa ni muhimu tukahimiza watu wetu kuchukua tahadhari," alisema Mayeka na kuongeza.

"Madiwani mnayo nguvu kubwa na mnasikilizwa na wananchi, tuwahimize wanaoishi kwenye maeneo ya mabonde wahame mapema, ni muhimu kuchukua tahadhali tusisubiri mpaka maafa yaje kutokea," aliongeza.

Pia aliagiza kila kata kutenga maeneo ya juu yatakayotumika kuwahifadhi watu watakaokumbwa na athari za mvua nyingi iwapo itatokea kama sehemu ya maandalizi ya kuwa na uhakika wa makazi ya muda kwa wananchi.

Hivyo, alihimiza wananchi kuandaa mbegu za mazao zinazostahimili kwenye maeneo yenye ardhi iliyo na maji mengi kwa kuwa yale yaliyozoeleka yanaweza kuharibiwa na mvua ijayo na kusababisha mavuno kuwa hafifu.

Alisema ili kuepuka kutokea kwa njaa ni muhimu wataalamu wa kilimo wakashauri mbegu zinazoweza kuwa msaada zikiwamo zile zinazokomaa kwa muda mfupi ili zitumike pale itakapoonekana mvua zimenyesha juu ya wastani.

Suala la wakulima kuzingatia kilimo cha maeneo ya juu alilipa uzito akisema itasaidia kuokoa mazao yao tofauti na mashamba yaliyopo kwenye mabonde aliyosema yanaweza kuharibiwa kwa kusombwa na maji ya mvua au kuzidiwa na unyevu.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Ramadhani Shumbi, aliwasihi madiwani kuzingatia agizo hilo akisema linalengo la kunusuru maisha ya wananchi, hivyo ni muhimu kila mmoja wao akalifanyia kazi.

Kadhalika, alitahadharisha maeneo yote ya migodi kuchukua tahadhari za hali ya juu ili kuepuka madhara ya watu kufukiwa kwenye mashimo na hivyo akasisitiza kwamba ikiwezekana baadhi ya shughuli zisimame kwa muda.

Vilevile, aliwataka wataalamu wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) wilayani hapa kujiandaa kukabiliana na miundombinu ya barabara ambayo inaweza ikaharibika kutokana na mvua hiyo na kusababisha wananchi kukosa mawasiliano.



Dereva bodaboda wilayani Rungwe, mkoani Mbeya, akisafirisha ndizi kutoka shambani kwenda Soko la Kalasha ambalo lilianzishwa kwa mbadala wa Soko la Kiwira wilayani humo mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanawake, wasichana 14,000 kupatiwa elimu ya ujasiriamali

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SHIRIKA la Amref Tanzania, limesema linakusudia kuwafikia wanawake na wasichana 14,000 wa mikoa ya Iringa na Njombe ili kuwapatia elimu ya ujasiriamali kwa lengo la kuwainua kiuchumi.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na mhandisi wa maji na usafi wa mazingira kutoka shirika hilo, Mturi James wakati wa uzinduzi wa mradi wa maji, usafi wa mazingira na uwezeshaji wanawake na wasichana katika jamii zinazolima kahawa na chai.

Alisema mradi huo unalenga kinamama na vijana kwa kuwawezesha kupitia shughuli mbalimbali za kiuchumi pamoja na kuwawezesha kupata huduma bora za afya, maji na kunawa mikono.

James alisema kuwa wanasaidia vikundi kwa kuvianzishia miradi mbalimbali ikiwamo utengenezaji wa sabuni ili kuweza kujikwamua kiuchumi.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Lusungu Mbede, alisema bado kuna mahitaji mengi katika jamii lakini uwezo wa rasilimali za kuweza kuwafikia zipo kidogo.

Meneja mradi kutoka Global Water Challenge, Domoina Randriamiarina, alisema wameweka mtazamo katika kuhakikisha wanawake wanawezeshwa.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Mji Njombe, Enembora Lema alisema halmashauri inafanya kazi nyingi kama vile kutoa mikopo, mafunzo lakini hawawezi kufikia watu wote.

Akisoma risala ya kikundi cha winner's, Lucia Lukas alisema changamoto ni kukosekana kwa soko la uhakika la bidhaa zao wanazozalisha kwa sababu hazina uthibitisho wa Shirika la Viwango la Taifa (TBS) na hivyo kusababisha kukosa wateja nje ya Mji wa Njombe.





## Mkazo wawekwa katika uimarishaji sekta ya mawasiliano

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema imeweka mkazo katika kuimarisha sekta ya mawasiliano ili kwenda sambamba na mabadiliko ya dunia.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohamed, aliyasema hayo juzi katika hafla ya uzinduzi wa bodi mpya ya Shirika la Mawasiliano Zanzibar.

Alisema serikali imeweka kipaumbele maalum katika kuimarisha huduma sahihi za teknolojia ya habari na mawasiliano kwa lengo la kuwajengea uwezo wananchi.

Waziri huyo alisema bodi hiyo itakuwa na jukumu kubwa la kusimamia sera za ICT, pamoja na kusimamia miundombinu, bajeti na matumizi ya shirika katika kuhakikisha malengo ya serikali yanafikiwa.

Pia alisema serikali imeona ipo haja ya kuanzisha shirika hilo ili kutoa nguvu zaidi kujiendesha kibiashara na kuongeza faida.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Mawasiliano Zanzibar, Dk. Mahmoud Abdulwahab Alawi, alisema atahakikisha shirika hilo linafikia malengo na madhumuni ya kuanzishwa kwake katika ukuaji na kujiendesha kwa kujitegemea.

Aidha, aliwataka wajumbe wa bodi hiyo pamoja na wafanyakazi kutoa ushirikiano hasa katika utendaji wa kazi zao za kila siku ili kufikia lengo la kutoa huduma bora za mawasiliano.

Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, Shukuru Awadhi Suleiman, alisema kuteuliwa kwa bodi hiyo kutasaidia kutoa msukumo katika utekelezaji wa miradi ya shirika hilo ambayo kwa sasa ipo katika mchakato wa utekelezaji.

Wajumbe wa bodi hiyo wameteuliwa kwa mujibu wa Sheria Namba 4 ya Mwaka 2023, ambao ni Dk. Mahmoud Abdulwahab Alawi ambaye ni mwenyekiti.

Wajumbe ni Said Seif Said, Mohamed Khamis Mussa, Abdulrahaman Ali Hassan, John Mahundi, Chai Ali Mohamed na Mhandisi Shukuru Awadhi Suleiman.

# Mkakati wa kupambana na VVU Zanzibar waandaliwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imeandaa Mkakati wa Nne wa Kitaifa wa Mapambano ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) 2023/2027, ambao utatekelezwa kwa kuangalia makundi hatarishi yakiwamo wanaofanya biashara ya ngono.

Pia utatekelezwa kwa wanaume wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja pamoja na watumiaji wa dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga sindano.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Omary Dadi Shajak, wakati akizungumza katika mdahalo wa mapambano ya Ukimwi.

Mdahalo huo uliwashirikisha askari wa vikosi vya serikali ya Zanzibar, uliandaliwa na Tume ya Ukimwi Zanzibar, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani ambayo huadhimishwa kila mwaka ifikapo Desemba Mosi.

Alisema bado maambukizi ya VVU kwa makundi hayo yapo juu visiwani Zanzibar, kwamba ni zaidi ya asilimia 0.1 ikilinganishwa na asilimia 0.4 ya maambukizi kwa watu wote Zanzibar.

Alisema mkakati uliopo ni kuyafanyia kazi makundi hayo ili yasiendelee kuambukiza na kufikia asilimia zero ya maambukizi mapya ifikapo mwaka 2030.

Alisema katika utekelezaji wa mkakati wa tatu wa kitaifa wa kupambana na Ukimwi, kuna changamoto zilijitokeza ikiwamo kutoyafikia makundi hayo hatarishi.

Aliwataka vijana hao kupambana na matumizi ya dawa za kulevya na maambukizi ya VVU ili kuishi bila ya kuwa na maambukizi hayo.

Akitoa mada ya elimu ya msingi kuhusu maambukizi ya VVU, Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Ukimwi Zanzibar, Ahmed Khatib, alisema Zanzibar ilianza kupata wagonjwa watatu waliogundulika kuwa na maambukizi ya VVU mwaka 1986.

Alisema wagonjwa hao waligundulika katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na kasi ya wagonjwa wa maradhi hayo ikazidi kuongezeka.

Alisema ilipofika mwaka 2005 Zanzibar iliungwa mkono na Serikali ya Marekani ambapo ilipatiwa dawa za kuwasaidia wanaoishi na VVU na dawa hizo zimesaidia kupunguza vifo na kasi ya maambukizi.

Alisema njia zinazosababisha kupata maambukizi ya VVU ni kujamiana na kati ya watu wote wanaoishi na maambukizi ya Ukimwi duniani asilimia 70 wamepata kwa njia hiyo.

Alitaja njia nyengine ni kuchangia damu ambayo haijafanyiwa uchunguzi na maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Aidha, alisema kwa sasa kasi ya maambukizi mapya ya VVU yamepungua Zanzibar na kwa sasa kasi hiyo imebaki kwa makundi hatarishi.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni (kulia), akisalimina na Mwakilishi wa Kidiplomasia wa Aga Khan Development Network nchini (AKDN), Amni Kurji, kabla ya kuanza kwa sherehe ya kumbukizi ya kuzaliwa kwa Mtume Muhammad iliyoandaliwa na Jumuiya ya Ismaili juzi jijin Dar es Salaam, wengine ni viongozi wa jumuiya hiyo. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# Serikali yataja faida ya takwimu nchi za Afrika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaban, amesema moja ya malengo ya takwimu za Afrika ni kutumika katika harakati za maendeleo hasa katika ukiukwaji wa masoko yake.

Alisema hayo jana katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Takwimu za Afrika.

Alisema Afrika imeweka siku hiyo ili kuangalia namna gani ya kukua kwa mipango yake ya kimaendeleo hasa katika sekta ya kibiashara na nchi wanachama kupiga hatua kiuchumi.

Alisema wakati umefika kwa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika kupanga mipango ya pamoja katika kufikia maendeleo kwa malengo ya kukua kiuchumi kwa nchi hizo.

Waziri Shaaban alisema katika kufikia maendeleo ya kweli lazima wananchi wa Afrika kujenga utamaduni wa kununua bidhaa zilizotengenezwa katika mataifa hayo ili kuunga mkono nchi zao.

Alisema nchi nyingi za Afrika wakati wa Uviko- 19 uchumi wao umeathirika kwa vile nchi hizo hutegemea bidhaa kutoka katika mataifa mengine ya nje.

Aidha, alisema kwa upande wa Zanzibar ikiwa moja ya nchi za Afrika hutumia takwimu katika mipango yake ya maendeleo na kuwasogezea wananchi wake huduma za kijamii.

Alisema Zanzibar ni moja ya nchi ambayo inapeleka mazao yake katika masoko ya Afrika na nje ya Afrika hasa karafuu ili kupata soko zuri, hivyo wakati umefika kuwa na ubunifu wa mazao mengine. Alisema katika kipindi cha miaka miwili ijayo Zanzibar inaenda kuongeza thamani ya mwani katika masoko ya Afrika na nje ya Afrika na hivi sasa serikali iko mwishoni kukamilisha kiwanda cha kusarifu mwani.

Alisema kiwanda hicho kinahitaji zaidi ya tani 300,000 kwa mwaka wakati hivi sasa siyo zaidi ya tani 12,000 zinazopatikana kwa mwaka.

Naye Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Salum Kassim Ali, alisema kabla ya kuadhimisha Siku ya Takwimu ya Afrika nchi wanachama wanakaa pamoja na kujadiliana juu ya mafanikio kupitia katika takwimu zao.

Alisema ni lazima Zanzibar kuchangamkia fursa ya soko hilo ili kuongeza thamani ya uchumi wake na wananchi kuendelea kupata maendeleo.

# Mifugo 300 yanaswa ikipelekwa nje ya nchi kwa njia za magendo

**Na Mwandishi Wetu,** LONGIDO

JESHI la Polisi kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia doria ya pamoja, limekamata watuhumiwa wawili wakiwa na jumla ya mifugo 303 ambayo walikuwa wanaisafirisha kwenda nje ya nchi kwa njia za magendo.

Akitoa taarifa hiyo kwenye maeneo ya Mnada wa Longido, Kamanda wa Polisi Kikosi cha Kuzuia Wizi wa Mifugo nchini, Kamishna Msaidizi Simon Pasua, alibainisha jana kuwa mifugo hiyo pamoja na watuhumiwa hao walikamatwa maeneo ya Buguruni C, Wilaya ya Longido, mkoani Arusha.

Kamanda Pasua alifafanua wanaendelea na upelelezi. Ukikamilika watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Alitoa wito kwa wafugaji nchini kuacha tabia ya kutorosha mifugo kwenda nje ya nchi bila ya kufuata utaratibu wa kupata vibali serikalini. Jeshi litachukua hatua za kisheria dhidi yao ikiwa ni pamoja na kukamata mifugo hiyo na kuwafikisha mahakamani.

Sambamba na hilo, pia alitoa rai kwa wafugaji kote nchini kutumia vizuri msimu huu wa mvua ambao kuna malisho ya kutosha, kutenga maeneo ya malisho ambayo watayatumia katika msimu wa kiangazi. Kutasaidia kuepukana na migogoro baina ya wafugaji na wakulima.

Daktari wa Mnada wa Longido, Dk. Ally Hamka, alisema changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni baadhi ya wafanyabiashara wa mifugo kutokuwa waaminifu kwa kukwepa kupeleka mifugo yao katika mnada huo kwa ajili ya kupewa vibali.

Alisema kuwa kupitia doria hiyo ambayo ni endelevu, watabaini na kuwakamata wafanyabiashara wanaotorosha mifugo na kuwachukulia hatua za kisheria.

Joseph Lengashe, mfugaji na mfanyabiashara, aliwaasa wafanyabiashara wenzake kufuata utaratibu ambao umewekwa na serikali wa kupata vibali vya kusafirisha mifugo yao ili kuepuka hasara ambazo wanaweza kukutana nazo pindi mifugo yao itakapokamatwa na kutaifishwa.




Mkuu wa Huduma za Pamoja wa Benki ya NMB, Nenyuata Mejooli (katikati), akizungumza na Rais wa Chama cha Makandarasi nchini, Mhandisi Judith Odunga (kushoto), katika mkutano kati ya Benki ya NMB na viongozi wa taasisi mbalimbali zinazoongozwa na wanawake jijini Dar es Salaam. Kulia ni Kaimu Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Ferdinand Mpona. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mamilioni yatolewa kutatua kero Shirika la Elimu Kibaha

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SERIKALI imeanza kutatua kero ya uchakavu wa miundombinu ya Shirika la Elimu Kibaha kwa kutenga fedha za maendeleo ya shirika hilo na kutoa fedha za ukarabati.

Kwa nyakati tofauti shirika hilo limekuwa linatoa taarifa ya uchakavu wa miundombinu yake ambayo kwa muda mrefu haijafanyiwa ukarabati.

Zaidi ya Sh. milioni 700 zimetengwa katika mwaka wa fedha 2023/24 kwa ajili ya kuboresha shirika hilo kwa kukabiliana na changamoto zilizopo ikiwamo uchakavu wa miundombinu.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Elimu Kibaha, Robert Shilingi, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya 51 ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii.

Alisema katika mwaka wa fedha 2023/24, serikali imetenga Sh. milioni 700 kwa shirika hilo kwa ajili ya kuboresha utoaji elimu. Kabla ya kutenga fedha hizo, serikali ilitoa Sh. milioni 400 za ukarabati wa miundombinu.

Mkurugenzi huyo alibainisha kuwa katika kipindi cha miaka mitatu, shirika hilo lilipokea Sh. bilioni 2.5 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, hatua ambayo imesaidia kupiga hatua za maendeleo katika utoaji elimu.

Awali akizungumza katika mahafali hayo, Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Joseph Nchimbi, alisema licha ya kufanikiwa kutoa elimu kwa wanafunzi na kuwapatia ujuzi katika fani mbalimbali ambazo zimewawezesha kujiajiri wenyewe, wamekuwa wanakabiliwa na vikwazo katika utekelezaji wa mipango yao.

Alibainisha vikwazo hivyo ni pamoja na uchakavu wa miundombinu, upungufu wa vifaa vya kutosha kufundishia, ukosefu wa samani za kutosha, lakini wamefanikiwa kupunguza wimbi la vijana kukosa ajira.

Mwenyekiti Halmashauri Mji wa Kibaha, Musa Ndomba, aliwataka wahitimu hao kutumia mafunzo waliyopata kujiajiri wenyewe na kutumia fursa za mikopo ya halmashauri ambayo inatolewa kwa vikindi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ili kujikwamua kiuchumi.

Akisoma risala kwa niaba ya wanafunzi waliohitimu, Asha Njooka, alisema chuo hicho kimetoa fani mbalimbali za ujasiriamali ambazo zitawasaidia kujiajiri na kuajiriwa, hatua ambayo itawaletea maendeleo na kujikwamua katika dimbwi la umaskini.

Shirika la Elimu Kibaha lilianzishwa mwaka 1964 na ni moja ya mashirika kongwe nchini yaliyoanzishwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere. Lilianzishwa likiwa na lengo la kupambana na maadui watatu; maradhi, ujinga na umaskini.

# Watoto walelewe kimaadili kuwaepusha na vitendo viovu

**Na Christina Haule,** MOROGORO

KUWALEA watoto katika misingi ya maadili mema kunaleta amani ya akili na moyo mtulivu kwenye familia na kuondoa mashaka kwa wazazi ya kuwa na vizazi vyenye matendo maovu ikiwamo unywaji pombe na uvutaji wa dawa za kulevya.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Morogoro, Rehema Malimi, alisema hayo jana kwenye sherehe za kitaifa za mwaka wa matendo ya huruma kwa jamii zilizoandaliwa na Shule ya Fountain Gate Accademy, mkoani hapa.

Malimi alisema ameona shule hiyo ikisaidia watoto katika maeneo manne muhimu ya malezi ambayo ni mahitaji ya mwili kwa wale wanaokosa kutoka kwa wazazi, imani katika kuongozwa kwenye dini, kuendeleza akili kwa kusoma na kusikiliza hisia za watoto kwa kukuza vipaji, kitendo ambacho mara nyingi hakitendewi haki kuanzia ngazi ya kaya.

Alisema bila malezi kila mtu asingekuwa hivyo alivyo sasa sababu wazazi au familia iliwekeza kwenye elimu kwa ajili ya mtoto na bila usimamizi mzuri baadaye mzazi ataanza kulalamika kuwa ana mtoto mwenye tabia za uvutaji bangi au unywaji pombe.

Aliwasisitiza viongozi wa shule hiyo kuhakikisha wanawapata wahitaji sahihi katika kuwapatia misaada na kuwahimiza wenye mali na vitu kujitoa kupitia taasisi kama hiyo ili kusaidia jamii na kuwa sadaka kamili yenye baraka mbele za Mungu.

Naye Mkurugenzi wa shule hiyo, Japhet Makau, alisema imejitolea kuwalea watoto walio kwenye shule zao na wenye uhitaji kwa kufuata misingi ya madili ikiwamo upendo.

Alisema pia hutumia miziki ya ndani wanayoiandaa wenyewe kwa ushirikiano wa walimu na wanafunzi na kutumika kwenye vipindi vya michezo badala ya miziki ya kileo ambayo imeonekana kuwaharibu watoto.

Mmoja wa watoto 38 waliofanikiwa kupata elimu kupitia shule hiyo, Winifrida Simon, aliwaomba wadau wengine kuwa na mioyo ya kusaidia wahitaji kwa sababu bado ni wengi.

Simon ambaye kwa sasa ni mwalimu kwenye shule hiyo, jijini Dar es Salaam aliishukuru taasisi hiyo kwa kumsaidia kielimu tangu kidato cha tano hadi chuo kikuu na kufanikiwa kupata nafasi hiyo baada ya kujiunga kama kibarua na baadaye kuingizwa kwenye orodha ya kupatiwa msaada.

# HABARI KIMATAIFA



Wapalestina wakitembea kuelekea ufua wa bahari ya Gaza baada ya kutoroka kwenye Hospitali ya Al-Shifa ambayo imezingirwa na majeshi ya Israel jana. **PICHA: MTANDAO**

## Kampeni za uchaguzi zaanza rasmi DRC

**KINSHASA,** DRC

KAMPENI za uchaguzi wa urais, wabunge na magavana zimeanza rasmi huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) huku wagombea 26 wakiwania kiti cha urais ambao wameanza kuzunguka maeneo mbalimbali nchini humo ili kuwashawishi wapigakura milioni 44 kuwachagua.

Inaelezwa kuwa wagombea hao watanadi sera zao kwa kipindi cha mwezi mmoja na kampeni zitahitimishwa Desemba 19, huku uchaguzi ukitarajiwa kufanyika Desemba 20, mwaka huu. Aidha, inaelezwa kuwa watu wengi huzungumza kuhusu kampeni hizo hasa katika nafasi ya kuchagua kati ya wagombea 26 wa urais.

"Tunasubiri kila mgombea aweze kuwasilisha sera zake za kampeni na mradi wake wa utawala, tutaona, tutathmini kile ambacho kila mmoja amezungmzia, tutaamua tumchague nani, alisema Edric, mmoja wa wakazi wa Kinshasa.

Mwananchi mwingine aliyejitambulisha kwa jina la Peter ambaye ni mmoja wa wasimamizi wa kampuni ya basi, alisema ana shauku kubwa baada ya kampeni za uchaguzi kuanza, akieleza kuwa inaonyesha uhai wa demokrasia nchini humo.

Ninajiamini sana kwa hilo, alisema. Alice, ambaye ni mwanafunzi, alisema atafuata kampeni, lakini zaidi ya yote anataka kura ya wazi.

Maana viongozi wakija kwa utapeli ni hatari sana kwetu. Wanakuja kwa maslahi yao wenyewe. Lakini viongozi wanapopata kura zao kwa haki, ni tofauti, alisema.

Hata hivyo ilielezwa kuwa licha ya kila mtu kudai kuwa ana kadi yake ya kupiga kura, lakini bado hawana uhakika kwamba watapiga kura Desemba 20.

Vile vile wagombea urais wanatarajia kunadi sera zao kwa wapigakura katika maeneo mbalimbali ya nchi hiyo, na kwamba Rais Félix Tshisekedi ameamua kuanza katika mji mkuu wa Kinshasa.

Pia ilielezwa kuwa wapinzani wake wakuu akiwamo Moïse Katumbi anatarajiwa kuwapo Kisangani, na Martin Fayulu atakuwa Bandundu katika ngome yake.

Ilibainishwa kuwa wagombea wengine wataenda mashariki mwa nchi hiyo, katika eneo linalokumbwa na migogoro. Hasa katika mpaka wa Kivu Kaskazini ambako maeneo ya Rutshuru na Masisi hayataweza kupiga kura kutokana na kuwepo kwa uasi wa M23.

Sio tu wagombea urais ambao watafanya kampeni, wagombea kwenye viti vya ubunge na kwenye nafasi za magavana wameanza pia kampeni zao jana. **RFI**

# Nchi tano zapeleka malalamiko ICC dhidi ya Israel

**GAZA,** Palestina

NCHI tano miongoni mwa zilizotia saini kuhusu kuundwa kwa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) zimeomba kufanyika kwa uchunguzi kuhusu hali katika eneo la Palestina kutokana na mashambulizi ya Israel yanayoendelea.

Hayo yamebainishwa na Mwendesha Mahakama hiyo, ambaye alibainisha kuchunguza kuhusu uhalifu uliofanywa tangu shambulio baya la Hamas la Octoba 7, mwaka huu, baada ya kupata malalamiko kutoka Afrika Kusini, Bangladesh, Bolivia, Comoro na Djibouti.

Afrika Kusini ilieleza kuwa imewasilisha malalamiko haya na nchi nyingine zinazotiwa wasiwasi na hali hii huko Palestina ili ICC ichukuwe hatua ya haraka kwa uzito wa hali ya sasa.

Aidha, Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi wa Kipalestina, (UNRWA) limetangaza kwamba shule ya pili imekuwa ikilengwa na mashambulizi kaskazini mwa Gaza. Na kwamba jengo hilo linatumika kama kimbilio salama ya zaidi ya watu 4,000 kutokana na mashambulizi ya Israel.

Jana Hamas ilitangaza kuwa Wapalestina 12,300 wameuawa katika mashambulizi ya anga ya Israel kwenye Ukanda wa Gaza tangu kuanza kwa vita. Na kwamba kati yao zaidi ya 5,000 ni watoto.

Ilibainishwa kuwa mamia ya watu walihamishwa Jumamosi kutoka Hospitali ya Al-Shifa, ambayo ni kubwa zaidi huko Gaza, kulingana na Umoja wa Mataifa, kulikuwa na wagonjwa wasiopungua 2,300, madaktari na watu waliokimbia makazi yao waliokwama kutokana na vita.

Wahudumu wa afya walisema wagonjwa 120, wakiwamo watoto wanaozaliwa kabla ya wakati, bado wako kwenye kituo hicho.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) linaonya kuhusu hatari ya haraka ya njaa katika Ukanda wa Gaza.

"Hatuulizi mwezi. Tunatoa wito wa kuchukuliwa hatua za kimsingi zinazohitajika ili kukidhi mahitaji muhimu ya raia na kukomesha hali ya janga hili," alisema mkuu wa operesheni za kibinadamu za Umoja wa Mataifa," Martin Griffiths.

### WATOROKA HOSPITALINI

Katika hatua nyingine Shirika la habari la (AFP) limetoa picha za msafara wa Wapalestina wanaotoroka hospitali ya Al-Shifa wakikimbilia maeneo mengine kwa miguu.

Hata hivyo ilielezwa kuwa mamia ya watu wanaripotiwa kuondoka katika hospitali hiyo, ambayo majeshi ya Israel yamekuwa yakiipekua kwa siku kadhaa.

Picha zilizowasilishwa na AFP zilionyesha wanaume, wanawake na watoto wakitembea kwenye mitaa iliyojaa vifusi huku tingatinga la kijeshi likiwa kwa nyuma.

Mwandishi wa AFP alisema umati huo ulijumuisha wagonjwa na majeruhi na walikuwa wakielekea kwenye ufuo wa bahari wa Gaza.

Awali iliripotiwa kuwa Wizara ya Afya inayoendeshwa na Hamas huko Gaza ilisema kulikuwa na wagonjwa 120 na idadi isiyojulikana ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati walioachwa katika kituo hicho.

Mkurugenzi wa hospitali alilishutumu Jeshi la Israel kwa kuamuru raia kuhama, lakini IDF ilisema ilisaidia kuwezesha ombi kutoka kwa mkurugenzi. **RFI, BBC**

HABARI MICHEZO

# BETWAY KUPELEKA WATANZANIA AFCON KUISHANGILIA TAIFA STARS

**Na Mwandishi Wetu**

KUPITIA Promosheni ya 'Twende AFCON' inayoendeshwa na Kampuni ya Betway Tanzania, mashabiki wa soka nchini wamepewa fursa ya kuwania tiketi ya kwenda Ivory Coast kushuhudia Timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars', ikichuana kuwania Kombe la Mataifa ya Africa (AFCON) 2023.

**Taifa Stars imefuzu kwa mara ya tatu kushiriki michuano hiyo itakayofanyika Januari mwakani nchini Ivory Coast na kwa kutambua umuhimu wa kuwaongezea morali wachezaji uwanjani, Kampuni ya Betway Tanzania imetangaza kupeleka mashabiki wanne kupitia kampeni hiyo ili kwenda kuishangilia.**

Katika kampeni hiyo ya mwezi mmoja iliyoanza rasmi Novemba 16 na kuendelea hadi Desemba 16, mwaka huu, lengo ni kuiongezea hamasa Taifa Stars pamoja na kuwapa watenja wake na mashabiki wa mchezo wa soka kwa ujumla nafasi ya kuwa sehemu ya historia ya soka la Tanzania.

Ili kushiriki katika promosheni hiyo, mshiriki anapaswa kujisajili na kubashiri mchezo wowote na Betway kwa kiwango cha kuanzia shilingi 100 kupitia mtandao wowote wa simu katika kipindi kati ya Novemba 16 na Desemba 16, mwaka huu na kila ubashiri utaingiza kwenye droo ya bahati, ambapo mshindi atajishindia tiketi ya kwenda Ivory Coast.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa promosheni hiyo iliyofanyika Ofisi za Betway jijini Dar es Salaam jana, Meneja Uendeshaji wa Betway Tanzania, Jimmy Masaoe, alisema wanafurahi kuwa sehemu ya historia ya mpira wa miguu nchini Tanzania kwa kuhakikisha Watanzania wanaiunga mkono Taifa Stars katika mashindano makubwa zaidi ya mpira barani Africa.

"Promosheni hii ni moja ya njia ya sisi kuisaidia timu yetu ya taifa na kutoa fursa kwa mashabiki kushuhudia mashujaa wa nchi wakipeperusha bendera huko Ivory Coast," alisema Masaoe.

Kwa upande wa Meneja Masoko wa Betway Tanzania, Calvin Mhina, aliwahimiza mashabiki wa michezo na wateja wa Betway kushiriki katika promosheni hiyo na kuitumia kama fursa ya kuiunga mkono timu ya taifa huku wakibashiri kistaarabu.

"Hii ni fursa ya kipekee na nzuri kwa wapenzi wa mpira wa miguu nchini Tanzania. Usikose nafasi hii ya kushinda tiketi kwenda AFCON na kushangilia Taifa Stars. Jisajili na Betway leo na weka ubashiri wako kuingia kwenye droo, unaweza kuwa mmoja wa washindi ya kwenda Ivory Coast na kuwa sehemu ya historia mpya katika soka la Tanzania.

"Kila shabiki anaweza kubashiri michezo anayoitaka na kuanzia kiwango cha chini kabisa cha shilingi 100. Tumefanya hivi ili kuhakikisha washiriki wanabashiri kistaarabu kama ambavyo kauli mbiu yetu imekuwa ikisisitiza," alisema Mhina.

Michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023, itafanyika nchini Ivory Coast kuanzia Januari 13 hadi Februari 11, 2024 ikijumuisha timu 24 zikiwania kombe hilo lenye thamani zaidi barani Africa.

Tanzania, baada ya kufuzu kwa mara ya tatu tu tangu ilipofuzu mwaka 1980 na 2019, itaanza kampeni yake katika Kundi F dhidi ya Morocco Januari 17, ikifuatiwa na mechi dhidi ya Zambia Januari 21 na kisha DR Congo Januari 24, mwakani.




Ofisa Uendeshaji wa Betway Tanzania, Jimmy Masaoe (katikati) pamoja Ofisa Masoko wa kampuni hiyo, Calvin Mhina (wa tatu kushoto) wakiwa pamoja na Ofisa Mkaguzi Mkuu wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (wa pili kulia), pamoja na mabalozi wa Betway; Idris Sultan (kulia), Salama Jabir (wa pili kushoto) na Geoffrey Lea (kushoto), wakiwa wameshika mfano wa Kombe la AFCON kama ishara ya safari ya kwenda kuiunga mkono Timu ya Taifa Tanzania, Taifa Stars, kuelekea fainali hizo Januari mwakani. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# KMC yazitaka tatu za Kagera Sugar

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa KMC FC, Abdihamid Moalini, amesema kikosi chake kipo imara na tayari kwa ajili ya kusaka alama tatu katika mchezo ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar utakaopigwa keshokutwa, Jumatano.

Amesema mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Al Hilal waliyocheza juzi, imewasaidia kuboresha changamoto za kikosi chake na kuwaamini vijana wake kwenda kupambana kusaka matokeo mazuri kwenye mchezo huo wa ugenini.

KMC FC tayari imewasili Bukoka, Kagera kwa ajili ya mchezo huo utakaopigwa katika Uwanja wa Kaitaba mkoani huo majira ya saa 1:00 usiku.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Moalini, alisema kikosi kipo imara baada ya kupoteza mechi yao ya mwisho nyumbani dhidi ya Dodoma Jiji FC, walirurudi uwanja wa mazoezi kufanyia kazi changamoto chache ikiwamo umakini wa safu ya ulinzi.

Alisema wameweza kusahihisha baadhi ya makosa yao baada ya kucheza mechi ya kujipima nguvu na Al Hilal ya Sudan na kuwa tayari kwa mchezo wao wa keshokutwa dhidi ya Kagera Sugar.

"Tumefanya maandalizi mazuri, tumesahihisha makosa yaliyojitokeza kwenye mechi iliyopita ambayo tulipoteza nyumbani dhidi ya Dodoma Jiji FC, tukacheza mechi ya kirafiki ya kimataifa, imetusaidia kwenye maandalizi yetu ya mchezo ujao dhidi ya Kagera Sugar.

"Ninaimani hautakuwa mchezo rahisi, utakuwa wa kimbinu na kiufundi kwa sababu kila mmoja wetu amefanya maandalizi mazuri, tunahitaji kupata matokeo mazuri ugenini," alisema Moalini.

Alisisitiza kuwa kikosi kipo imara na vijana wako tayari kwa ajili ya kupambania alama tatu muhimu ili kujiweka kwenye nafasi ya nne ya msimamo wa ligi hiyo.

Katika msimamo wa Ligi Kuu, KMC FC iko nafasi ya tano chini ya Dodoma Jiji FC na wote wamekusanya alama 15 katika michezo tisa ambayo tayari timu zote zimecheza kasoro Simba na Mashujaa FC zilizopo nyuma mechi moja.

# KMKM na ndoto za ubingwa Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya kuchezea kichapo juzi, kikiwa ni cha nne tangu kuanza kwa msimu huu, Kocha Msaidizi wa KMKM SC, Ame Msimu, amesema kupoteza mchezo huo dhidi ya vinara wa Ligi Kuu, JKU SC, haina maana kama wamejitoa katika mbio za kutetea ubingwa wao.

KMKM SC iliendelea kupoteza matumaini ya kutetea taji lao la Ligi Kuu Zanzibar baada ya juzi kuchezea kichapo cha mabao 2-1 dhidi ya Maafande wa JKU SC katika mwendelezo wa ligi hiyo ikiwa mzunguko wa 11.

Ushindi huo kwa JKU uliirudisha kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kwa kuwa na alama 26 huku KMKM SC ikiendelea kusalia nafasi ya tano na alama zake 17.

Akizungumza na Nipashe juzi, Kocha Msaidizi wa KMKM, Msimu alisema kupoteza mchezo huo dhidi ya vinara wa Ligi kuu haina maana kama wamejitoa katika mbio za kutete ubingwa wao na kwamba bado wanaamini wanaweza kufanya vizuri na kutwaa taji hilo.

Alisema mara nyingi mzunguko wa kwanza unakuwa mgumu zaidi kwa kuwa kila timu inahitaji kupata alama ambazo zitamhakikishia anakuwa katika nafasi nzuri kabla ya kuanza mzunguko wa lala salama.

Alisema kwa upande wao, KMKM matokeo ya kufungwa katika michezo yao waliyocheza kumetokana na ligi yenyewe kuwa ngumu hasa katika mzunguko huu wa kwanza.

Alisema katika mchezo wao huo dhidi ya JKU timu zote zilicheza vizuri kwa kuwa kila timu inahitaji kupata alama tatu ili kuendelea na safari ya kuusaka ubingwa msimu huu, lakini bahati haikuwa upande wao.

"Tulicheza vizuri sana, wachezaji walijituma dakika zote 90, lakini tulikutana na timu ambayo nayo inausaka ubingwa na sisi tumo katika hesabu hizo, hivyo lazima mchezo kuwa mgumu licha ya sisi kumiliki mpira, lakini nadhani haikuwa bahati yetu kupata alama tatu," alisema.

Aidha, alisema katika mchezo wao ujao wa 12 dhidi ya Mafunzo, watahakikisha wanacheza kwa mipango mizuri ili kupata alama tatu.

KMKM imepoteza jumla ya michezo minne, imetoka sare miwili na imeshinda mitano kati ya 11 iliyocheza hadi sasa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DE GEA AKATAA MAMILIONI

GOLIKIPA wa zamani wa Hispania, David de Gea, 33, amekataa mkataba utakaomfanya alipwe mshahara wa pauni 500,000 kwa wiki na fursa ya kuunganishwa na mchezaji mwenzake wa zamani wa Manchester United, Cristiano Ronaldo, Klabu ya Saudia ya Al-Nassr. ***(Sun)***

### ATAKIWA PIA INTER MIAMI

INTER Miami ni moja ya klabu zinazompa David De Gea fursa ya kurejea kwenye soka lake huku akiwa hana klabu baada ya kuondoka Manchester United msimu uliopita. ***(Star)***

### PHILLIPS NA WEST HAM

KLABU ya West Ham imeungana na Newcastle United katika kinyang'anyiro cha kumnunua Kalvin Phillips, 27, huku Manchester City wakiwa tayari kumruhusu kiungo huyo wa kati wa England kuondoka kwa mkopo au kwa mkataba wa kudumu dirisha la Januari. ***(Football Insider)***

### WERNER BASI TENA

KLABU ya Fulham ina uwezekano wa kutafuta chaguo lingine kabla ya kufikiria uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa RB Leizpig na Ujerumani, Timo Werner, 27, Januari. ***(Football Insider)***

### MODRIC KUHAMIA SAUDIA

KIUNGO wa kati wa Croatia, Luka Modric, 38, ameamua kuhamia Saudia wakati mkataba wake na Real Madrid utakapokamilika msimu wa majira ya ujao. ***(Sport)***

### GUIRASSY AWANIWA

KLABU ya Newcastle United inajaribu kumnunua mshambuliaji wa Stuttgart kutoka Guinea, Serhou Guirassy, 27. ***(Football Insider)***

### SALANKE ATAJWA WEST HAM

KLABU ya West Ham inatazamia kufufua tena azma yao ya kumnunua mshambuliaji wa Bournemouth, Dominic Solanke, 26. ***(Mirror)***

### MILLER ANYATIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur, Aston Villa, Newcastle United, Brighton, Brentford na West Ham ni miongoni mwa zinazomfuatilia kwa karibu kiungo wa kati wa Motherwell, Lennon Miller, 17. ***(Teamtalk)***

### BELLINGHAM MDOGO SOKONI

KLABU ya Tottenham Hotspur pia inamfuatilia kwa karibu kiungo wa Sunderland, Jobe Bellingham, 18, ambaye ni mdogo wake Jude. ***(Football Insider)***


### VELIZ ALENGWA SPURS

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur, Alejo Veliz, 20, analengwa na Klabu ya Serie A ya Bologna, huku mshambuliaji huyo wa Argentina akiwa ameshindwa kupata namba chini ya kocha, Ange Postecoglou tangu alipotua hapo akitokea Rosario Central. ***(Calciomercato)***

### NUSA ATAKIWA FULHAM

KLABU ya Fulham inapanga kumnunua mshambuliaji kinda wa Club Bruges na Norway, Antonio Nusa, 18 katika dirisha la Januari. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SANCHO HANA MPANGO KWENDA KUCHEZA SAUDIA

**MANCHESTER,** England

**Mwenyewe ataka kurejea tena Borussia Dortmund, lakini United inataka...**

WAWAKILISHI wa Jadon Sancho wamesisitiza kuwa fowadi huyo hatalazimishwa kuondoka Manchester United hadi ofa kubwa itakapotolewa, huku kukiwa na nia ya kutoka Ulaya na Saudi Arabia.

**90min inaelewa kuwa Sancho anatakiwa kuondoka United katika dirisha la usajili la Januari licha ya mchakato wa Sir Jim Ratcliffe kununua hisa asilimia 25 za klabu hiyo.**

Sancho ameondolewa kwenye kikosi cha kwanza baada ya kutofautiana na Kocha Erik ten Hag kutokana na kufungwa na Arsenal mwanzoni mwa msimu, ambapo alidai kuwa mchezaji huyo wa Kimataifa wa England aliachwa nje ya kikosi cha siku ya mechi kutokana na kuonesha kiwango kidogo mazoezini.

Sancho alijibu kwa taarifa ya umma ya kumkaidi kocha wake kwenye mtandao wa Kijamii wa X (zamani Twitter).

United ilithibitisha mzozo huo kwamba Sancho aliondolewa kwenye kikosi cha kwanza na imebakia kuwa hivyo tangu wakati huo, na 90min iliripoti wiki kadhaa zilizopita kwamba uhusiano wao haukuweza kurekebishwa.

Ten Hag ametaka Sancho kuomba msamaha ili kurekebisha hali hiyo, lakini hakujawa na dalili zozote za kutokea na hakuna uwezekano wa kutokea wakati huu.

Klabu kadhaa zimeonesha nia ya kumnunua mchezaji huyo tangu mwaka jana, ikiwa ni pamoja na msimu uliopita wa majira ya joto na United inataka kiasi kikubwa cha fedha ili kumuuza.


Kuondoka kwa mkopo kunaonekana kuwa na uwezekano zaidi kwa wakati huu, huku Sancho akiwa hana uhakika na Klabu za Saudi Arabia.

Wawakilishi wa Sancho wameweka wazi kwa United kwamba watachagua uhamisho mwingine wa Sancho, ingawa baadhi ya nyuso tofauti zinaweza kufanya maamuzi ndani ya kuta za Old Trafford ifikapo mapema 2024.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, anapendelea kurejea katika klabu yake ya zamani ya Borussia Dortmund, ambayo alijiunga nao mwaka 2021.

Klabu hiyo ya Bundesliga ingehitaji kutoa nafasi kwenye kikosi chao ili kumchukua Sancho na kuna uwezekano mkubwa wa kumchukua kwa mkopo, lakini Sancho angehitaji United kubadilika ili kufanya uhamisho huo.

# HAALAND 'KUFUNGWA' UPYA MAN CITY




**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City inaendelea kushinikiza mazungumzo na wawakilishi wa Erling Haaland kuhusu mkataba mpya, kwa mujibu wa 90min.

Nyota huyo wa Norway ameendeleza mafanikio ya msimu wake wa kwanza wa ajabu nchini England, ambapo City ilishinda taji la Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA, na kuwa kileleni mwa orodha ya wafungaji mabao kwa mabao 17 katika mechi 18 katika michuano yote.

Haaland amejidhihirisha kama mshambuliaji mkuu katika soka la dunia tangu ajiunge na City, akionesha kwamba mabao yake ya awali kule Borussia Dortmund na Red Bull Salzburg hayakuwa ya bahati mbaya, na msimamo wake kwenye mchezo huo ulithibitishwa alipomaliza kama mshindi wa pili wa Ballon d'Or nyuma ya Lionel Messi.

Alitia saini mkataba wa miaka mitano alipojiunga na City msimu wa majira ya joto wa 2022, na mkataba huo ukijumuisha vipengele kadhaa kama alivyokuwa Dortmund na Salzburg.

Amekuwa akihusishwa na Real Madrid na Barcelona tangu wakati huo, na wengi wanahisi kuwa hatima ya Haaland ni kuishia katika moja ya Klabu za Hispania.

90min ilifichua Machi mwaka huu kwamba City walikuwa wameiambia kambi ya Haaland kuhusu nia yao ya kuondoa kipengele maalum cha kuachiwa kutoka kwenye mkataba wake - huku wakijadiliana kuhusu masharti mapya na yaliyoboreshwa.

Lakini wakapewa mkwamo mfupi na wakala wake, Rafaela Pimenta, ambaye anatamani Haaland mwenye umri wa miaka 23, kuwa katika udhibiti wa maisha yake ya baadaye.

Real Madrid wametajwa kuwa ndio wanaopewa nafasi kubwa ya kumsajili Haaland, ikiwa ataondoka, lakini mipango yao bado inahusu kujaribu kumsajili Mbappe kutoka PSG msimu ujao wa joto.

# Vinicius miezi 2 nje ya dimba

**MADRID,** Hispania



MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Vinicius Junior, atakuwa nje ya uwanja kutokana na jeraha la misuli ya paja, klabu hiyo ya LaLiga ilithibitisha juzi, na kupata pigo jingine kwa timu hiyo ambayo tayari ina wachezaji kadhaa majeruhi wa muda mrefu msimu huu.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba anatarajiwa kutopatikana kwa karibu miezi 2 na nusu. Jeraha hilo ni kubwa kuliko tatizo la msuli wa paja katika mguu wake mwingine lililomweka nje kwa mwezi mmoja kati ya Agosti na Septemba mapema msimu huu.

Vinicius mwenye umri wa miaka 23, alilazimika kutoka nje kutokana na jeraha la paja wakati Brazil ilipofungwa mabao 2-1 na Colombia katika mechi ya kufuzu kwa Kombe la Dunia Alhamisi na alirejea katika klabu yake kwa uchunguzi zaidi.

"(Vinicius) amegundulika kuwa kaumia katika sehemu ya paja ambayo inaathiri mshipa wake," ilisema taarifa ya Real Madrid.

"Kupona kwake kutafuatiliwa."

" Tutarudi na nguvu zaidi," aliandika Vinicius kwenye ukurasa wake wa X.

Vinicius ana mabao sita na asisti nne katika mashindano yote kwa Madrid msimu huu.

Real Madrid pia wamempoteza kiungo Eduardo Camavinga mwenye umri wa miaka 21, kutokana na jeraha akiwa kwenye majukumu ya kimataifa, akiwa amechanika mshipa katika goti lake la kulia alipokuwa akifanya mazoezi na Ufaransa.

Camavinga amecheza katika kila mechi ya ligi kwa Real msimu huu, na anaungana na Thibaut Courtois, Eder Militao na Arda Guler kwenye orodha ya wachezaji wa Madrid ambao wamepata majeraha ya goti.

# Kane aweka rekodi ya mabao England

**LONDON,** England

HARRY Kane amejidhihirisha kuwa mmoja wa washambuliaji wakubwa wa England na sasa ameweka rekodi ya kuwa mfungaji bora zaidi wa nchi hiyo.

Nahodha Kane alifunga bao la pili katika ushindi wa England wa mabao 2-0 dhidi ya Malta katika Uwanja wa Wembley, huku Simba Watatu hao wakiwa tayari wamehakikishiwa nafasi ya kucheza Euro 2024.

Kane sasa amefunga mabao 62 katika mechi 88 alizoichezea England juu ya Wayne Rooney akiwa kileleni mwa orodha ya wachezaji wenye mabao mengi zaidi kwa nchi hiyo.

Bao lake la kwanza kwa England lilikuwa ni mechi yake ya kwanza, alipoingia kama mchezaji wa akiba dhidi ya Lithuani.

Kane mwenye umri wa miaka 30, ana hat-trick tano kwa England kwa jina lake.

Mara yake ya kwanza ilikuwa dhidi ya Panama kwenye Kombe la Dunia 2018, na alifunga mabao matatu dhidi ya Bulgaria na Montenegro katika kufuzu kwa Euro 2020 mwaka mmoja baadaye.

Mwaka 2021 alifunga hat-trick mfululizo dhidi ya Albania na San Marino katika kufuzu Kombe la Dunia ugenini kuelekea Qatar.

Mikwaju yake 21 ya penalti ndiyo jumla ya juu zaidi iliyopigwa na nyota yeyote wa England.

Wafungaji watano bora wa England ni Kane (62), Wayne Rooney (53), Bobby Charlton (49), Gary Lineker (48) na Jimmy Greaves (44).



# CAFWCL yawapa jeuri JKT Queens

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa JKT Queens, Esther Chabruma, ameweka wazi kuwa michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika (CAFWCL), imekuwa na zoezi tosha kwao kuwasaidia kufanya vizuri msimu huu kwenye michezo iliyopo mbele yao ikiwamo Ngao ya Jamii na Ligi Kuu Tanzania Bara.

JKT Queens ni Mabingwa Watetezi wa Ligi Kuu Bara na hivi karibuni waliondolewa katika michuano ya CAFWCL katika hatua ya makundi nchini Ivory Coast na timu hiyo, imerejea kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu unaotarajiwa kuanza Desemba 15 au 16, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, kocha huyo alisema kikosi chake kimerejea mazoezini kujiandaa na msimu mpya wa ligi hiyo na anaamini watafanya vizuri na kutetea taji lao la ubingwa huku wakihitaji kutwaa Ngao ya Jamii.

Alisema anaimani kubwa ya kufanya vizuri kwa sababu michuano ya kimataifa imewasaidia kutokana na kukutana na timu bora na kufanya vizuri jambo ambalo linawapa kuendeleza makali yao msimu unaoanza.

"Ligi haitakuwa rahisi, ninaimani kubwa michuano ya kimataifa imeweza kutusaidia kuona ubora wa timu yetu ukizingatia tumecheza na timu bora katika michuano hiyo, imetusaidia na kujiandaa kwa Ngao ya Jamii na kufanya vizuri kwenye ligi," alisema kocha huyo.

Timu hiyo iko kambini kwa ajili ya msimu mpya ambapo Desemba 8, mwaka huu, kutakuwa na michuano ya Ngao ya Jamii ambayo itakuwa ni mara ya kwanza kwa upande wa kufanyika nchini kwa upande wa wanawake.

**Ligi haitakuwa rahisi, ninaimani kubwa michuano ya kimataifa imeweza kutusaidia kuona ubora wa timu yetu ukizingatia tumecheza na timu bora katika michuano hiyo...**

# MFUNGAJI BAO TAIFA STARS AFUNGUKA, KOCHA ALONGA

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa Timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars', aliyefunga bao pekee juzi katika mechi ya kwanza ya Kundi E kusaka tiketi ya kucheza Kombe la Dunia mwaka 2026, Charles M'mombwa, ameeleza kufurahishwa kufunga bao lake la kwanza akiichezea timu hiyo, pamoja na sapoti kubwa aliyoipata kutoka kwa mashabiki ambayo hakuitegemea.

M'mombwa, mwenyeji wa Kigoma kwa sasa anacheza soka la kulipwa katika Klabu ya Macarthur FC nchini Australia, alifunga bao pekee dakika 11 baada ya mapumziko, kwenye Uwanja wa Marrakech nchini Morocco dhidi ya Niger na kuipatia pointi tatu za ugenini katika safari ya kusaka tiketi ya kucheza fainali hizo zitakazochezwa kwenye nchi tatu za Marekani, Canada na Mexico.

**"Nina furaha sana, nashukuru mashabiki wa Tanzania kwa sapoti, nashukuru sana, tutaendelea kupambana kwa ajili ya taifa nadhani lengo letu litafanikiwa," alisema mchezaji huyo anayecheza winga wa kushoto.**

Alipachika bao hilo lililoanzia nyuma kwa Bakari Mwamnyeto ambaye alipiga mpira mrefu ambao uliangukа katikati ya wachezaji wa timu mbili na katika kunyang'anyana, nahodha Mbwana Samatta aliudhibiti mpira na kuupeleka kwenye wingi ya kushoto, ukamkuta mfungaji ambaye alivuta hatua chache na kuachia shuti la mguu wa kushoto lililombabatiza beki mmoja wa Niger na kujaa wavuni.

Kocha Mkuu wa Stars, Adel Amrouche, alisema ushindi huo utawapa morali Watanzania na wachezaji kwa ajili ya mechi zinazofuata, akisema ni mwanzo tu wa safari ndefu ya kuisaka tiketi hiyo.

"Wachezaji walicheza vizuri, walifuata maelekezo, haikuwa mechi rahisi lakini kwa ushirikiano wa watu wote waliokuja nchini Morocco, tumepata ushindi.

"Huu ni mwanzo kwa sababu safari ni ndefu na mechi za mbele ni ngumu zaidi, lakini kinachofurahisha ni kupata ushindi wa ugenini," alisema.


Niger inacheza kwenye uwanja huo wa Morocco kutokana na viwanja vya nchini kwao kutokidhi vigezo vilivyowekwa na Shirikisho la Soka Duniani, FIFA.

Kocha huyo aliishukuru serikali kwa kutoa ndege maalum ya kuwapeleka na kuwarudisha, akisema imewapa morali na kuwarahishia kurejea haraka kwa ajili ya mechi nyingine kesho dhidi ya Morocco.

"Tunamshukuru sana Rais wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutupa ndege, vinginevyo tungekuwa na safari ndefu sana, kwa usafiri wa Afrika kutoka Mashariki kwenda Magharibi ni mbali sana na hata kurejea kucheza dhidi ya Morocco ingekuwa shida sana," alisema kocha huyo.

Kwa matokeo hayo, Stars imekwea hadi nafasi ya pili ya msimamo wa Kundi E ikiwa na pointi tatu na bao moja, huku kinara wa kundi akiwa ni Zambia ambayo iliibamiza Congo Brazaville mabao 4-2, mechi ikichezwa Uwanja wa Levy Mwanawasa, Ndola, Zambia.

Stars imerejea nchini na inatarajia kujitupa kesho, Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Timu ya Taifa ya Morocco.



Mkuu wa Uendeshaji NBC, Alelio Lowassa (kushoto), akikabidhi mpira kwa Mwalimu wa Michezo wa Shule ya Sekondari Tambaza ya jijini Dar es Salaam, Nicholaus Nolasco, ikiwa ni moja ya zawadi zilizotolewa na benki hiyo kwa uongozi na wanafunzi wa shule hiyo wakati semina fupi ya mafunzo kuhusu elimu ya fedha na akiba iliyoendeshwa na benki hiyo shuleni hapo jana. Wanaoshuhudia ni pamoja na Mkuu wa Shule hiyo, Hussein Mavumba (wa pili kushoto), walimu, wanafunzi na maofisa wengine waandamizi wa benki hiyo. **MPIGAPICHA WETU**

# *Gamondi aiandalia 'sapraizi' Belouizdad*

INATOKA UKURASA 24

"Kikosi kipo vizuri licha ya wachezaji wengine kuwapo kwenye majukumu ya timu zao za taifa, waliobaki wanafanyia kazi majukumu yao ili kujiweka imara zaidi ya mechi zilizopita," alisema kocha huyo.

Alisisitiza kuwa wamejiandaa kwa mapambano ya aina yote kwa kila mchezaji kufanya kazi kwa ushirikiana mkubwa ili kufikia malengo wanayoyatarajia kwa msimu huu.

Kocha huyo alisema anachohitaji ni kupata ushindi katika mchezo wa kwanza, na kwamba anaamini akianza vizuri haitokuwa kazi kubwa kwenye michezo inayofuata.

Wachezaji wa timu hiyo walipata mapumziko ya siku moja na leo wanarejea kwenye uwanja wa mazoezi kuendelea na maandalizi ya mechi hiyo ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

# Cadena aanza kupata dawa

INATOKA UKURASA 24

wakipendekeza Che Fondoh Malone achezeshwe kama kiungo mkabaji, hawakukosea kwani alianza kuifungia timu hiyo bao la kwanza dakika ya 40, akipata pasi kutoka kwa Mohamed Hussein 'Tshabalala.'

Willy Onana, ambaye inasemekana huenda akaonyeshwa mlango wa kutokea kipindi cha dirisha dogo kwa kushindwa kuwashawishi mabosi wake na hata mashabiki, alifunga bao la pili kwa mkwaju wa penalti, Israel Patrick akifunga bao la tatu kabla ya Moses Phiri kuhitimisha idadi ya mabao kwa kufunga la nne dakika ya 75 baada ya kupokea pasi ya kisigino kutoka kwa nahodha John Bocco.

Simba inaelekea kwenye mechi hiyo ya hatua ya makundi bila kocha mkuu, ambapo ndoto za kumpata kabla ya mechi hiyo kama ilivyokuwa inadaiwa na viongozi wa klabu hiyo zinaelekea kufifia.

# Michezo

Jumatatu Novemba 20, 2023

Nipashe





Sancho hana mpango na Saudia UKURASA 21

KITU HICHO...



Kiungo wa Simba, Fabrice Ngoma, akijaribu kufunga kwa kichwa huku kipa wa Dar City, akijiandaa kudaka, kwenye mechi ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Simba Mo Arena, Bunju, Dar es Salaam jana. Simba ilishinda 4-0. **PICHA: SIMBA**

# Gamondi aiandalia 'sapraizi' Belouizdad

**Na Saada Akida**

## ●●● Ataka kwenda kuishangaza kwao huku akieleza tayari amekisuka kikosi chake kwa...

HUKU mastaa wake wengine wakiwa katika majukumu ya timu za taifa, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema anatarajia 'sapraizi' kwa kufanya mabadiliko ya kikosi chake katika mchezo wa kwanza wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria.

**Kikosi cha Yanga kinaendelea na maandalizi ya mchezo huo watakaokuwa ugenini Ijumaa wiki hii katika Uwanja wa Julai 5, 1962 (Stade du 5 Juillet 1962) nchini humo kuhakikisha wanaanza vizuri hatua ya makundi.**

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema ana matarajio ya kuingia katika mchezo huo kwa mbinu nyingine tofauti ikiwamo kufanya mabadiliko ya kikosi kwa sababu anatambua CR Belouizdad nao wamekuwa wakifuatiliwa tangu makundi yalipopangwa.

Alisema licha ya wao kuwafuatilia CR Belouizdad katika michezo yao, pia Yanga wamekuwa wakifuatiliwa kwa umakini, hivyo atahakikisha anafanya mabadiliko ya kikosi katika mchezo huo wa ugenini.

"Mabadiliko ya kikosi yatakuwapo, wachezaji watakapokamilika wote kila mmoja atakuwa anajua majukumu yake, katika mchezo huo hatutaingia kama ilivyo kwa michezo mingine tuliocheza awali," alisema Gamondi.

Aliongeza kuwa yuko makini katika kuimarisha kikosi chake katika kila sekta zaidi washambuliaji ambao tayari amefanyia kazi na sasa yupo na safu ya ulinzi kulingana na uimara wa washambuliaji wa CR Belouizdad.

"Nimewafuatilia baadhi ya michezo yao wakicheza, nao wamefanikiwa kufunga bao kila mechi, hilo tuko nalo makini kuhakikisha tujiweke sawa kila eneo na kuwakumbusha mabeki kuwa makini.

INAENDELEA UKURASA 23

# Cadena aanza kupata dawa ya mabeki Simba SC

**Na Adam Fungamwango**

KUELEKEA kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast Jumamosi ijayo, inaonekana kama Kaimu Kocha Mkuu, Daniel Cadena, ameanza kupata dawa ya mabeki wa Simba kuruhusu mabao katika mechi zote wanazocheza baada ya kutoruhusu nyavu zake kutikiswa jana katika mchezo ya kirafiki dhidi ya Dar City kwenye Uwanja wa Mo Arena, wakishinda 4-0.

Cadena, ambaye baada ya kuichukua Simba iliyokuwa chini ya Roberto Oliveira aliyeondoshwa kutokana na kipigo cha mabao 5-1 Novemba 5, mwaka huu, alibainisha wazi kuwa katika jambo linalomkera ni timu hiyo kuruhusu bao na mabao karibuni kwenye kila mechi inayocheza iwe ya Ligi ya Mabingwa, African Football League, Ligi Kuu Tanzania Bara na hata mechi za kirafiki.

Baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Namungo kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, kocha huyo aliainisha ni kitu gani ataanza nacho kwenye mazoezi na kinaonekana kimeanza kufanyiwa kazi.

"Kwa sasa kazi yangu kubwa kuelekea kwenye mchezo ujao ni kuisuka beki, nataka kupunguza baadhi ya makosa na mapungufu ya kuruhusu mabao, kwa timu kubwa kama yetu si vema kuwa na tabia hiyo kwa sababu mara kwa mara tunacheza na timu kubwa ambazo hutumia makosa madogo ambayo yanafanyika kukuadhibu," alisema.

Jana asubuhi, Cadena alionekana kusisitiza kukaba kwa ushirikiano, huku mabeki wakitakiwa kutofanya makosa ya kujirudia.

Kwenye mechi hiyo ya kirafiki, kocha aliwachezesha baadhi ya wachezaji ambao wamekuwa hawapati nafasi kama Abdallah Khamis, David Kameta na Nassor Kapama.

Wadau wa soka wakiongozwa na rais wa zamani wa Simba, Ismail Aden Rage, waliokuwa

INAENDELEA UKURASA 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >